**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**











# Mpango Mkakati wa Kisayansi wa Kujenga Umahiri wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa Watoto wa Elimu ya Awali na Wanafunzi wa Darasa la Kwanza na la Pili



**Januari, 2026**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

# MPANGO MKAKATI WA KISAYANSI WA KUJENGA UMAHIRI WA KUSOMA, KUANDIKA NA KUHESABU (KKK) KWA WATOTO WA ELIMU YA AWALI NA WANAFUNZI WA DARASA LA KWANZA NA LA PILI

**JANUARI, 2026**

## YALIYOMO


VIFUPISHO....................................................................................................iii
SHUKRANI ...................................................................................................iv
DIBAJI.......................................................................................................... v
1.0 UTANGULIZI.............................................................................................. 1
1.1 Dhana ya Sayansi katika Mkakati wa Kuimarisha Umahiri wa KKK ................. 1
1.2 Hali Ilivyo ................................................................................................... 6
1.2.1 Muktadha wa Sera za Kitaifa.................................................................... 7
1.2.2 Sera za Kikanda na Kimataifa ................................................................ 11
1.3 Uchambuzi wa Uwezo, Udhaifu, Fursa na Changamoto ............................... 15
1.3.1 Uwezo wa Ndani ya Mfumo..................................................................... 16
1.3.2 Udhaifu ................................................................................................ 17
1.3.3 Fursa .................................................................................................... 17
1.3.4 Changamoto na Vikwazo vya Nje ya Mfumo ........................................... 18
1.4 Sababu, Mantiki na Uhalali wa Mkakati ....................................................... 19
1.5 Dira na Dhima ............................................................................................ 21
1.5.1 Dira ya Mkakati ..................................................................................... 21
1.5.2 Dhima ya Mkakati .................................................................................. 21
1.6 Malengo, Kanuni, Maadili na Wigo .............................................................. 22
1.6.1 Malengo ................................................................................................ 22
1.6.2 Kanuni Elekezi ...................................................................................... 23
1.6.3 Wigo wa Utekelezaji................................................................................ 24
2.0 MPANGO MKAKATI ................................................................................... 25
2.1 Nguzo Kuu na Maeneo ya Kimkakati ........................................................... 25
2.1.1 Elimu ya Awali Jumuishi na Ujifunzaji Unaomlenga Mtoto.................... 26
2.1.2 Kuimarisha Uwezo wa Walimu na Mazingira ya Ufundishaji wa Stadi za KKK ........................................................................................................ 27
2.1.3 Kuimarisha kipindi cha Mpito Endelevu na Jumuishi katika Ujifunzaji wa Stadi za KKK kutoka Elimu ya Awali hadi Darasa la Kwanza na la Pili . 28
2.1.4 Kuimarisha Tathmini ya Ujifunzaji na Afua za Kurekebisha Ujifunzaji wa Stadi za KKK) ........................................................................................ 29
2.1.5 Kuimarisha Mifumo ya Takwimu, TEHAMA na Maamuzi Yanayotokana na Ushahidi katika Ujifunzaji wa Stadi za KKK ..................................... 30
2.1.6 Kuimarisha Ustawi, Ulinzi na Mazingira Wezeshi ya Ujifunzaji kwa Watoto wa Elimu ya Awali na Darasa ya la Kwanza na la Pili .............. 31
2.1.7 Kuimarisha Uongozi, Uratibu, Ufadhili Endelevu na Uwajibikaji katika Utekelezaji wa Mkakati wa Stadi za KKK ............................................ 32
3.0 BANGO KITITA LA MKAKATI WA KISAYANSI WA KUIMARISHA STADI ZA KKK ......................................................................................................... 34
4.0 UFUATILIAJI NA TATHMINI ...................................................................... 80
4.1 Malengo Mahsusi ya Ufuatiliaji na Tathmini ................................................. 80

4.2 Maeneo na Vipengele Muhimu vya Ufuatiliaji na Tathmini.............................. 81
5.0 MPANGO ENDELEVU WA MKAKATI.......................................................... 83
MAREJELEO ......................................................................................... 91

# VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| AU | - | *African Union* |
| AZAKI | - | Asasi za Kiraia |
| ADEM | - | Agency for the Development of Educational Management |
| BEMIS-SIS | - | *Basic Education Management Information System- School Information Systems* |
| CESA | - | *Continental Education Strategy for Africa* |
| EAC | - | *East African Community* |
| ESDP | - | *Education Sector Development Plan* |
| FAO | - | *Food and Agriculture Organization* |
| INSET | - | *In-Service Education and Training* |
| ISW | - | Institute of Social Work |
| JzK | - | Jumuiya za Kujifunza |
| KKK | - | Kusoma, Kuandika na Kuhesabu |
| MMK-KKK | - | Mpango Mkakati wa Kisayansi wa Kuimarisha Stadi za KKK |
| NECTA | - | *The National Examinations Council of Tanzania* |
| NM-ECDP | - | *National Multisectoral Early Childhood Development Programme* |
| OWM-TAMISEMI | - | Ofisi ya Waziri Mkuu- Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| PJT-MMMAM | - | Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto |
| PSLE | - | *Primary School Leaving Examination* |
| RUCU | - | Ruaha Catholic University Management |
| SADC | - | *Southern African Development Community* |
| SDGs | - | *Sustainable Development Goals* |
| TaRL | - | *Teaching at the Right Level* |
| TEHAMA | - | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TET | - | Taasisi ya Elimu Tanzania |
| TEWW | - | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima |
| UNDG | - | *United Nations Development Group* |
| UNESCO | - | *United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization* |
| UNICEF | - | *United Nations Children's Fund* |
| UWaWa | - | Ushirikiano wa Walimu na Wazazi |
| WFP | - | *World Food Programme* |
| WMJJWM | - | Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wanawake na Makundi Maalum |
| WyEST | - | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia |

## SHUKRANI

Kwa heshima na taadhima kubwa, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia anapenda kutoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri, maono ya mbali na dhamira ya dhati katika kuimarisha Sekta ya Elimu nchini. Uongozi wa Mheshimiwa Rais umeendelea kuweka kipaumbele katika uwekezaji wa Elimu ya Msingi, hususan Elimu ya Awali, kama nguzo muhimu ya maendeleo ya rasilimali watu na ustawi wa Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Waziri pia anatoa shukrani za pekee kwa wadau wote wa elimu waliotoa mchango wao katika maandalizi ya Mpango Mkakati wa Kisayansi wa Kujenga Umahiri wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa Watoto wa Elimu ya Awali na Wanafunzi wa Darasa la Kwanza na la Pili. Miongoni mwa wadau hao ni Wizara na Taasisi za Serikali, Walimu, Watafiti, Wadau wa Maendeleo, Sekta Binafsi, pamoja na Wazazi na Jamii kwa ujumla. Kwa namna ya pekee niwashukuru wafuatao walioshiriki moja kwa moja kuandika mkakati huu: Prof. Ladslaus L. Mnyone, Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa, Abdul M. Maulid, Victor E. Bwindiki, Edward A. Wawa, Musa Swila, Dkt. Richard M. Chiligati, Tezra C. Mkama, Astheria Lwena, Tumaini Majula, Vaileth F. Chalamila, Magali Janneth Mwocha, Anna Godwin (WyEST); Allo J. Missai (OWM-TAMISEMI); Aurelia Msanga (WMJJWM); Boniface Mwaitenga na Salumu Chivalavala (NECTA); Joyce Chamuhulo (TET); Prof. Sotco C. Komba (ISW); Gladys Masyole (ADEM); Leonia Kassamsa (TEWW); na Dkt. Salvius Aloyce Kumburu (RUCU).

Mchango wa wadau hawa kupitia tafiti, uzoefu wa kitaalamu, ushauri na maoni ya kina umeiwezesha Serikali kuandaa Mpango Mkakati huu kwa kuzingatia ushahidi wa kisayansi, muktadha wa Tanzania, pamoja na misingi ya ubora, usawa na ujumuishi katika ujifunzaji wa watoto. Ushirikiano huu umechangia kwa kiasi kikubwa kubaini changamoto zilizopo, kupendekeza mikakati madhubuti ya utekelezaji, na kuweka mwelekeo wa pamoja wa kuboresha umahiri wa KKK katika madarasa ya Awali, Kwanza na Pili.

Mwisho, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia anatoa shukrani kwa jamii kwa kuendelea kushirikiana na Serikali katika malezi, ulinzi na ujifunzaji wa watoto na Wanafunzi wa Darasa la Kwanza na la Pili, akitambua kuwa mafanikio ya Mpango Mkakati huu yatategemea kwa kiasi kikubwa mshikamano na ushirikiano wa wadau wote. Serikali ina imani kuwa kwa juhudi za pamoja na uongozi thabiti, Mpango Mkakati huu utakuwa nyenzo muhimu katika kujenga msingi imara wa elimu bora na maendeleo endelevu ya Taifa letu.

Prof. Carolyne I. Nombo
**KATIBU MKUU**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

## DIBAJI

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua kwa dhati umuhimu wa kuimarisha umahiri wa Stadi za msingi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa watoto wa Darasa la Elimu ya Awali na Darasa la Kwanza na la Pili. Katika dunia ya leo inayobadilika kwa kasi, uwezo wa mtoto kumudu Stadi hizi za msingi mapema ndiyo nguzo ya mafanikio ya baadae ya kielimu, kijamii na kiuchumi. Hivyo, ni wajibu wetu kama Taifa kuweka msingi imara wa ujifunzaji unaozingatia ushahidi, ubora, usawa na ujumuishi kwa watoto wote.

.

Mpango Mkakati wa Kisayansi wa Kuimarisha Umahiri wa Stadi za KKK umeandaliwa ili kuelekeza utekelezaji wa afua zinazothibitishwa kitaaluma na kitaalamu, zinazolenga kuboresha matokeo ya ujifunzaji kwa Watoto wa Darasa la Awali na Darasa la Kwanza na la Pili. Mpango huu unasisitiza matumizi ya mbinu bora za ufundishaji na ujifunzaji, maendeleo endelevu ya walimu, upatikanaji wa nyenzo stahiki za kujifunzia, tathmini endelevu ya maendeleo ya wanafunzi, pamoja na ushirikishwaji wa wazazi na jamii katika malezi na ujifunzaji wa mtoto.

Mpango Mkakati huu unaongozwa na malengo mapana ya sera na miongozo ya Taifa katika sekta ya elimu, na umeandaliwa kwa kuzingatia ushahidi wa tafiti, tathmini za kitaifa, na uzoefu wa utekelezaji wa programu za Elimu ya Awali. Mafanikio yake yatategemea utekelezaji madhubuti wa mikakati iliyobainishwa na ushirikiano wa karibu kati ya wadau wote muhimu wakiwemo Wizara, Taasisi za Elimu, Walimu, Watafiti, Wadau wa Maendeleo, Sekta Binafsi, Jamii na Wazazi.

Katika kuandaa Mpango Mkakati huu, Serikali ilishirikisha wadau mbalimbali ili kuhakikisha kuwa unajibu ipasavyo mahitaji halisi ya muktadha wa Tanzania, na kwamba unalenga kupunguza tofauti za umahiri wa KKK, kuongeza usawa wa fursa za kujifunza, na kuboresha ubora wa ufundishaji na ujifunzaji katika Darasa la Awali, la Kwanza na la Pili. Mpango huu unatoa mwelekeo wa pamoja kwa wadau wote kuhusu kile kinachohitajika ili kuleta matokeo chanya na endelevu katika ujifunzaji wa KKK.

Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ina matumaini kuwa Mpango Mkakati huu utatumika kama mfumo thabiti wa kuongoza utekelezaji wa afua zenye tija, na hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa katika kujenga msingi imara wa elimu bora na maendeleo ya rasilimali watu kwa Taifa letu.

Mhe. Prof. Adolf Faustine Mkenda (MB)

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

# 1.0 UTANGULIZI

Ufanisi wa ufundishaji na ujifunzaji katika ngazi zote za elimu nchini unategemea kwa kiwango kikubwa msingi unaowekwa katika miaka ya mwanzo ya mtoto, hususan Elimu ya Awali na Darasa ya I–II. Tafiti za kitaalamu, ikiwemo uchambuzi wa Heckman (2006) mshindi wa Tuzo ya Nobel zinaonesha kuwa uwekezaji katika miaka minane ya mwanzo huleta tija kubwa zaidi kiuchumi, kijamii na katika maendeleo ya binadamu kuliko hatua nyingine yoyote ya elimu. Katika kipindi hiki ndipo Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK), tabia, maadili, na mielekeo ya mtoto hujengwa, na hivyo kuathiri kwa kiasi kikubwa mafanikio yake ya baadaye shuleni na katika maisha.

Kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa Stadi za KKK kwa watoto wa elimu ya msingi ni nguzo muhimu sana katika kujenga msingi imara wa ujifunzaji na maendeleo ya rasilimali watu nchini. Changamoto ya kumudu Stadi hizi za msingi imeendelea kuathiri uwezo wa baadhi ya watoto kuendelea na masomo ya ngazi za juu, hivyo kuhitaji hatua za haraka za kimkakati na zinazoongozwa na ushahidi wa kisayansi.

Katika muktadha huo, Serikali imeandaa mkakati madhubuti wa Kisayansi unaolenga kuhakikisha kuwa kila mtoto anaweza kumudu Stadi za KKK aingiapo Darasa la Tatu. Mwelekeo huu wa kitaifa ulisisitizwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akizindua Bunge la Kumi na Tatu mnamo tarehe 14 Novemba, 2025, ambapo alibainisha vipaumbele vya utekelezaji wa Serikali katika kipindi cha siku 100 za kwanza alipotoa maelekezo mahususi ya kuimarisha msingi wa elimu nchini. Katika kutekeleza agizo hilo, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iwe imeandaa na kuendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Kisayansi wa kufanya umahiri wa Kusoma Kuandika na Kuhesabu (MMK-KKK) ifikapo mwaka 2030.

## 1.1 Dhana ya Sayansi katika Mkakati wa Kuimarisha Umahiri wa KKK

Dhana ya Sayansi katika mkakati huu, inachukuliwa kwa mtazamo mpana unaojumuisha maamuzi yanayotegemea

ushahidi wa tafiti, tathmini ya mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji, na siyo matokeo ya mitihani pekee. Inahusisha umahiri wa walimu, ubora wa nyenzo, matumizi ya teknolojia, mbinu za ufundishaji na ufanisi wake katika kuleta matokeo chanya ya ujifunzaji. Msingi wa Kisayansi wa Mkakati wa Kitaifa wa KKK umejengwa juu ya sayansi ya maendeleo ya mtoto, nadharia za ujifunzaji, tafiti za kielimu, na matumizi ya takwimu katika maamuzi ya kisera na kiutendaji. Unatumia mtazamo jumuishi unaogusa vipengele vyote muhimu vinavyoathiri ujifunzaji wa mtoto. Ufafanuzi wa kina kuhusu sayansi inayokusudiwa katika mpango mkakati huu umetolewa kama ifuatavyo;

**(i) Ushahidi wa Kitaaluma na Uzoefu wa Ndani na Kimataifa.**

Mkakati umejikita katika tafiti zilizothibitishwa, falsafa za wataalamu wa sayansi ya ujifunzaji, na uzoefu wa Tanzania na kimataifa. Hivyo, utekelezaji wake unategemea ushahidi wa kisayansi badala ya mazoea au maoni binafsi.

**(ii) Ujifunzaji wa Awali kama Msingi wa Maendeleo ya Mtoto.**

Kwa kuzingatia ushahidi kwamba ukuaji mkubwa wa ubongo hutokea kabla ya miaka 8, mkakati unaweka mkazo katika Elimu ya Awali na madarasa ya I–II ili kujenga msingi imara wa kusoma, kuandika na kuhesabu mapema.

**(iii) Matumizi ya Mbinu zilizothibitishwa Kisayansi.**

Mkakati unapendekeza mbinu zilizojaribiwa kama ufundishaji unaozingatia uwezo wa ujifunzaji -*Teaching at the Right Level* (TaRL) na ujifunzaji unaozingatia michezo, ambazo zimeonesha kuimarisha umahiri, ushiriki na motisha ya wanafunzi katika mazingira yanayofanana na Tanzania.

(iv) **Tathmini Endelevu na Maamuzi yanayotegemea Takwimu.**

Mkakati unasisitiza tathmini za mara kwa mara, ukusanyaji wa takwimu sahihi, na matumizi ya ushahidi katika kupanga na kuboresha afua za kielimu ili kutatua changamoto za ujifunzaji mapema. Matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), teknolojia nyingine za kidijitali sambamba na mifumo ya takwimu za elimu, ikiwemo Basic Education Management Information System- School Information Systems (BEMIS-SIS) na mfumo wa kidijiti wa Uthibiti Ubora wa Shule ili kuwezesha ufuatiliaji wa matokeo ya ujifunzaji wa Stadi za KKK kwa wakati halisi na kufanya maamuzi yanayotegemea ushahidi pamoja na kutoa afua stahiki kwa mwanafunzi sahihi ili kutatua tatizo husika.

(v) **Mtazamo wa Maisha yote katika Ujifunzaji wa KKK.**

Ujifunzaji wa mtoto unaangaliwa kama mchakato endelevu unaoanzia nyumbani, kuendelea Elimu ya Awali na kuimarishwa katika madarasa ya mwanzo, kwa kuzingatia kuwa uwekezaji wa mapema huleta matokeo makubwa na endelevu.

(vi) **Ufuatiliaji, Tathmini na Uboreshaji Endelevu**

Mkakati unatumia mzunguko wa kisayansi wa uboreshaji endelevu (kupanga,kutekeleza, kupima, kutathmini na kuboresha) ili kuhakikisha utekelezaji unabaki kuwa hai, unaojifunza na unaojibu changamoto mpya kwa ufanisi.

Mkakati huu umejengwa juu ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 (Toleo la 2023, Dira ya maendeleo ya Taifa 2050 na Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu (ESDP 2025-2030). Nyaraka hizi zinasisitiza umahiri wa walimu katika kuwezesha ujifunzaji, matumizi ya mbinu shirikishi na bunifu, pamoja na matumizi ya TEHAMA katika kujenga Stadi za karne ya 21. Aidha, mkakati huu unatekeleza azma

ya taifa ya kujenga jamii iliyoelimika, yenye ujuzi na uwezo wa kushindana katika uchumi wa kisasa.

MMK-KKK unatumia nadharia inayosisitiza mabadiliko ya kifikra, kimtazamo na kimwelekeo, *Change Theory* (United Nations Development Group (UNPG) 2017) katika kufanikisha utekelezaji jumuishi wa programu yoyote ile. Hata hivyo, ushahidi wa kitaaluma unaonesha wazi kuwa ufanisi wa ujifunzaji katika ngazi yoyote ya elimu hutegemea kwa kiasi kikubwa msingi unaowekwa katika miaka ya mwanzo ya maisha ya mtoto, hususan katika elimu ya awali. Katika kipindi hiki ndipo Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu, pamoja na tabia, maadili na mielekeo ya mtoto hujengwa, na hivyo kuathiri kwa kiasi kikubwa mafanikio yake ya kielimu na maisha ya baadae (Ha, Lien & Hang,2025).

Takwimu za Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA) zinaonesha kupungua kwa idadi ya wanafunzi wasiomudu Stadi za KKK katika Darasa la Nne kwa kipindi cha miaka 2022 hadi 2024; hata hivyo, mafanikio haya yanaonesha jitihada za Serikali katika kuendelea kukabiliana na changamoto za ujifunzaji zinazojitokeza katika madarasa ya elimu ya awali.

Matokeo ya Upimaji wa Taifa wa Stadi za KKK kwa Darasa la Pili mwaka 2023 yanaonesha kuwa, ingawa asilimia 78.92 ya wanafunzi walipata utendaji wa wastani hadi mzuri katika Kusoma, viwango vya umahiri vilikuwa vya chini katika Kuandika (asilimia 69.63) na Kuhesabu (asilimia 62.56). Aidha, uchambuzi wa mwenendo wa upimaji wa Stadi za KKK kwa kipindi cha mwaka 2021 hadi 2023 unaonesha kuwa zaidi ya theluthi moja ya wanafunzi hawafikii viwango vya kitaifa vinavyokusudiwa, huku tofauti za umahiri zikiendelea kujitokeza kati ya maeneo ya mijini na vijijini. Mwelekeo huu unaashiria kuwa changamoto za ujifunzaji huanza mapema katika madarasa ya chini bila afua za mapema na zinazoongozwa na ushahidi

wa kisayansi, kuendelea kujirudia na kuathiri uwezo wa wanafunzi kuelewa masomo ya ngazi za juu, ikiwemo ufaulu katika Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi. Hivyo basi, mkakati huu wa kisayansi unatarajia kutatua changamoto za ujifunzaji na ufundishaji wa watoto wa madarasa ya Elimu ya Awali ili waweze kumudu Stadi za KKK wafikapo darasa la tatu.

Utekelezaji wa Mkakati huu pia ni sehemu ya mwitikio wa kitaifa kwa maazimio ya kikanda na kimataifa, hususan Mkutano wa Elimu wa Umoja wa Afrika (AU) wa mwaka 2024; uliosisitiza umuhimu wa kuongeza na kuboresha uwekezaji katika Elimu ya Awali kama njia ya kuondoa ujifunzaji duni (*learning poverty*). Umoja wa Afrika umezitaka nchi wanachama kuhakikisha upatikanaji wa walimu wenye sifa na uwajibikaji, mafunzo endelevu, vifaa vya kufundishia na kujifunzia, mazingira bora ya kazi, pamoja na kuharakisha upanuzi wa mbinu zilizothibitishwa kitaaluma kama *Teaching at the Right Level (TaRL)/Catch-Up* katika kuboresha ujifunzaji wa Stadi za msingi.

Mkakati huu una jukumu la kukuza ujifunzaji wa Stadi za KKK kwa kushirikisha wazazi, walezi na jamii katika kuhakikisha watoto wanajengewa mazingira wezeshi ya kujifunza nyumbani na shuleni.

Mkakati wa Kitaifa wa Kuimarisha Umahiri wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) umejengwa juu ya misingi imara ya kisayansi inayotokana na tafiti za maendeleo ya ubongo wa mtoto, sayansi ya ujifunzaji na ushahidi wa kielimu. Tafiti zinaonesha kuwa ujifunzaji wa awali ni msingi muhimu wa maendeleo ya kielimu ya mtoto, hivyo mkakati unaweka mkazo katika Elimu ya Awali na madarasa ya mwanzo (awali hadi darasa la pili) ili kuhakikisha watoto wanajengewa Stadi za msingi za KKK mapema. Mkakati unatumia mbinu za ufundishaji zilizothibitishwa kitaaluma, ikiwemo ufundishaji unaolingana na kiwango halisi cha mwanafunzi, ujifunzaji shirikishi na unaotegemea

michezo, ambazo zimeonesha kuongeza uelewa, ushiriki na motisha ya watoto katika kujifunza kusoma, kuandika na kuhesabu.

Aidha, mkakati wa kisayansi unasisitiza tathmini endelevu ya ujifunzaji, matumizi ya takwimu halisi katika kupanga na kuboresha afua, pamoja na ufuatiliaji na maboresho ya mara kwa mara ya utekelezaji. Mbinu hii ya kufanya uamuzi unaotokana na ushahidi huwezesha kubaini changamoto za ujifunzaji mapema, kutoa msaada lengwa kulingana na mahitaji ya wanafunzi, na kufuatilia maendeleo ya ujifunzaji kwa njia inayopimika. Kupitia mzunguko endelevu wa kupanga, kutekeleza, kupima na kuboresha afua, mkakati unabaki kuwa wenye ufanisi, unaojifunza kutokana na matokeo na unaoweza kujibu kwa ufanisi changamoto za utekelezaji wa KKK nchini Tanzania.

Kwa ujumla, Mpango Mkakati wa MMK-KKK unalenga kuimarisha Stadi za KKK na kuweka msingi imara wa ujifunzaji wa watoto/wanafunzi wa Kitanzania, kama nyenzo muhimu ya kufanikisha maendeleo ya rasilimali watu, ubunifu na ushindani wa Taifa, kwa mujibu wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050. Changamoto ya wanafunzi wasiomudu umahiri wa Stadi za KKK zimeendelea kubainika, jambo linaloweza kuathiri uwezo wa wanafunzi kumudu umahiri wa masomo ya ngazi za juu, ukiwemo ufaulu usioridhisha katika mtihani wa kumaliza elimu ya msingi.

## 1.2 Hali Ilivyo

Mkakati huu umeandaliwa katika muktadha mpana wa Sera, mipango na ajenda za maendeleo za Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ili kuhakikisha kuwa kila mtoto anapofika Darasa la Tatu anamudu Stadi za msingi za KKK. Mkakati unatambua kuwa ujifunzaji wa awali na wa msingi ni nguzo ya maendeleo ya rasilimali watu, ushindani wa kiuchumi na ustawi wa jamii kwa ujumla. Kupitia ulinganifu wake na Dira ya Taifa ya

Maendeleo 2050, Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 (Toleo la 2023), Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu (ESDP) 2025/26–2029/30 na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) (2025–2030), mkakati huu unaweka msisitizo katika kuboresha matokeo halisi ya ujifunzaji, kupunguza ujifunzaji duni (*learning poverty*) na kuhakikisha kuwa hakuna mtoto anayeachwa nyuma katika hatua za mwanzo za elimu.

Aidha, mkakati huu unaendana kikamilifu na Programu Jumuishi ya Kitaifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (PJT-MMMAM), pamoja na ajenda za kikanda na kimataifa zinazotambua na kuhimiza uwekezaji wa mapema katika maendeleo ya mtoto kama msingi wa maendeleo endelevu.

### 1.2.1 Muktadha wa Sera za Kitaifa

#### *1.2.1.1 Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050*

Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 inaelekeza Tanzania kujenga “jamii iliyoelimika, yenye ujuzi, inayopenda kujifunza na yenye uwezo wa kushindana” katika uchumi wa kisasa. Nguzo ya pili ya Dira, inayohusu *Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii*, inasisitiza uwekezaji mkubwa katika elimu ya msingi kama chachu ya maendeleo ya rasilimali watu. Mkakati huu wa kuhakikisha kila mtoto aliyefika darasa la tatu anamudu Stadi za msingi za KKK unatekeleza kwa vitendo dira hii kwa kuweka msingi imara wa ujifunzaji wa baadaye na kuondoa ujifunzaji duni (learning poverty), ambao ni kikwazo kikubwa kwa maendeleo endelevu ya taifa. Mkakati wa Kisayansi wa KKK ni nyenzo ya utekelezaji wa Dira ya Taifa 2050 katika sekta ya elimu, kwa kuwa unajenga msingi wa rasilimali watu yenye ujuzi, maarifa na uwezo wa kushiriki

kikamilifu katika uchumi unaotegemea sayansi, teknolojia na ubunifu.

#### 1.2.1.2 *Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014,Toleo la 2023*

Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, Toleo la 2023, imeweka mkazo katika ubora wa elimu, ujifunzaji unaojenga umahiri, na kuhakikisha watoto wote wanapata Stadi za awali za msingi tangu ngazi ya awali. Sera inatambua kuwa elimu ya Awali, Darasa la I na II ndiyo msingi wa kujifunza katika maisha yote, na inasisitiza Serikali kuhakikisha mitaala, walimu, mazingira ya kujifunzia na tathmini endelevu vinachangia katika kuwawezesha watoto kumudu mapema Stadi za KKK. Aidha, Mkakati huu unatekeleza moja kwa moja matamko ya sera yanayolenga kuboresha ujifunzaji halisi na wenye kujikita katika matokeo ya ujifunzaji badala ya kujikita katika uandikishaji na mahudhurio shuleni pekee.

#### 1.2.1.3 *Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu (*Education Sector Development Plan-ESDP*) 2025/2026–2029/2030*

Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu (ESDP) 2025/2026–2029/2030 umebainisha changamoto ya kushuka kwa viwango vya ujifunzaji wa msingi, hususan katika Stadi za KKK katika Elimu ya Awali na msingi. Mpango huu unaweka kipaumbele katika:

(i) Kuboresha ubora wa ufundishaji na ujifunzaji darasani;

(ii) Kuimarisha mifumo ya tathmini ya ujifunzaji; na

(iii) Kuwajengea walimu uwezo wa kufundisha kwa kuzingatia uwezo halisi alionao mwanafunzi.

Mkakati huu unaendana kikamilifu na vipaumbele vya ESDP kwa kulenga matokeo ya ujifunzaji, matumizi sahihi ya takwimu za tathmini, na mbinu zilizothibitishwa kama *TaRL* ili kuwasaidia wanafunzi ambao wameshindwa kumudu Stadi za KKK kufikia viwango vilivyowekwa.

#### *1.2.1.4 Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2025–2030)*

Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2025 – 2030 imeweka msukumo katika kuinua ubora wa elimu katika ngazi zote, kwa msisitizo maalumu katika Elimu ya Awali na msingi. Ilani inasisitiza pia kuwa taifa haliwezi kujenga uchumi imara na wenye ushindani bila watoto wake kumudu Stadi za msingi za kujifunza. Hivyo, Mkakati huu ni tafsiri ya kisera na ahadi ya Chama Tawala ya kuwekeza katika elimu bora, jumuishi na yenye matokeo, kwa kuhakikisha kuwa hakuna mtoto anayevuka hatua za mwanzo za elimu bila kumudu Stadi za KKK.

#### *1.2.1.5 Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (PJT-MMMAM 2021/2022-2025/2026)*

Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (PJT-MMMAM) inalenga kutatua changamoto za ukuaji na maendeleo ya watoto wenye umri kuanzia miaka 0 hadi 8, pia kutoa huduma jumuishi za Afya bora; lishe; ulinzi na usalama; malezi yenye mwitikio; na fursa ya

ujifunzaji wa awali kwa watoto. Programu hii inatambua pia kuwa maendeleo ya mtoto hayawezi kushughulikiwa na sekta moja pekee, bali yanahitaji ushirikiano wa sekta mbalimbali hususan Elimu, Afya, Ustawi wa jamii, Maji, Lishe na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

MMMAM inasisitiza fursa ya ujifunzaji wa awali kwa mtoto na malezi yenye mwitikio ili kuimarisha Stadi za KKK kwa mtoto na;

(i) kuongeza utayari wa mtoto kuanza shule;

(ii) kupunguza utoro na mdondoko wa wanafunzi;

(iii) kujenga msingi wa mafanikio ya ujifunzaji wa KKK; na

(iv) kuchangia ustawi wa mtoto kimwili, kijinsia, kiakili na kijamii.

Hivyo, mkakati wowote wa kuboresha ujifunzaji wa awali unapaswa kuzingatiwa kama sehemu ya utekelezaji wa MMMAM na siyo jitihada ya elimu pekee. Programu Jumuishi ya Kitaifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto, (PJT-MMMAM) huweka msingi wa maendeleo ya awali ya mtoto, wakati Mkakati wa Kisayansi wa KKK huendeleza na kuimarisha uwezo huo katika Elimu ya Awali na msingi. Kwa pamoja, mipango hii miwili inajenga mnyororo endelevu wa maendeleo ya rasilimali watu nchini.

### 1.2.2 Sera za Kikanda na Kimataifa

#### *1.2.2.1 Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 (SDGs)*

Mkakati huu unasadifu kikamilifu Lengo Na. 4 katika Malengo ya Maendeleo Endelevu (Sustainable Development Goals), hususan Kiashiria cha 4.1.1. Kiashiria hiki kinalenga kuhakikisha watoto wote wanapata matokeo bora ya ujifunzaji katika Kusoma na Kuhesabu. Lengo dogo la 4.2 linalozitaka nchi kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2030, watoto wote wawe wanapata huduma bora za Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali (MMAM) ili kuwa tayari kuanza elimu ya msingi. Mkakati wa Kisayansi wa KKK unatekeleza kwa vitendo malengo haya kwa kuimarisha ujifunzaji wa awali (*Foundational Learning*), unaojumuisha Stadi wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu kama msingi wa kujifunza maisha yote.

Aidha, Mkakati wa KKK una mchango wa moja kwa moja katika utekelezaji wa malengo mengine ya Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) yanayohusiana na ustawi wa mtoto, ikiwemo Lengo la 1 linalohusu Kutokomeza Umaskini kwa kuvunja mnyororo wa umaskini wa kizazi hadi kizazi kupitia ujuzi wa msingi. Lengo la 2 linalohusu Kutokomeza Njaa na Kukuza Lishe Bora kwa kutambua mchango wa lishe katika maendeleo ya ubongo na uwezo wa kujifunza. Lengo la 3 linalohusu Afya Njema na Ustawi kwa kuhusisha Afya ya awali na utayari wa mtoto kujifunza. Lengo la 5 linalohusu Usawa wa Kijinsia kwa kuhakikisha wasichana na wavulana wanapata fursa sawa za ujifunzaji wa msingi tangu awali.

Kwa kuzingatia ushahidi wa kisayansi unaoonesha kuwa uwekezaji katika miaka ya awali ya maisha ya mtoto huleta faida kubwa za kijamii na kiuchumi katika maisha ya baadaye. Mkakati wa KKK unaweka mkazo katika kuimarisha Elimu ya Awali na ujifunzaji wa msingi kama nguzo muhimu ya maendeleo endelevu. Vilevile, mkakati huu unaweka msingi thabiti wa upimaji na ufuatiliaji wa matokeo ya ujifunzaji yanayotambuliwa kimataifa, hususan kupitia Kiashiria cha SDG 4.1.1, na hivyo kuifanya Tanzania kufuatilia kwa ushahidi maendeleo ya watoto katika kusoma, kuandika na kuhesabu kwa viwango vinavyokubalika kimataifa.

#### *1.2.2.2 Ajenda ya Umoja wa Afrika (AU Agenda 2063 na AU Education Agenda 2024 –2034)*

Ajenda ya Umoja wa Afrika, kupitia Agenda 2063 na AU *Continental of Education Strategy for Africa* (CESA) pamoja na mwito wa Muongo wa Elimu Afrika (2024–2034), inasisitiza kuwa Afrika inahitaji kuwekeza mapema katika maendeleo ya mtoto ili kujenga rasilimali watu yenye ujuzi, ubunifu na uwezo wa kushindana AU inaweka mkazo maalum katika:

(i) kuondoa ujifunzaji duni (*learning poverty)*;

(ii) kuhakikisha watoto wanamudu Stadi za KKK katika hatua za mwanzo;

(iii) kuimarisha ubora wa walimu wa Elimu ya Awali na msingi; na

(iv) kupanua majaribio yaliyothibitishwa ya kuboresha ujifunzaji wa awali kama *Teaching at the Right Level (TaRL)*.

Aidha, Mkakati huu unalenga ujifunzaji wa awali na kutekeleza kwa vitendo maono ya AU ya “Afrika yenye watu walioelimika, wenye ujuzi na wanaochangia maendeleo ya bara”.

#### ***1.2.2.3 Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC)***

Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kupitia itifaki yake ya Elimu na Mafunzo (*SADC Protocol on Education and Training)* na mikakati yake ya maendeleo ya rasilimali watu, inazitaka nchi wanachama kuimarisha ubora wa elimu ya msingi kama msingi wa ujifunzaji wa maisha yote na ushindani wa kikanda. SADC inatambua kuwa changamoto ya ufaulu katika Stadi za KKK kwa madarasa ya awali ni kikwazo kikubwa kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya kikanda. Katika muktadha huu, SADC inaelekeza nchi wanachama:

(i) kuwekeza katika Elimu ya Awali na msingi kama nguzo ya maendeleo ya rasilimali watu;

(ii) kuimarisha mafunzo ya awali na endelevu kwa walimu wa elimu ya msingi;

(iii) kuboresha mifumo ya tathmini ya ujifunzaji ili kupima umahiri halisi wa wanafunzi; na

(iv) kukuza ushirikiano wa kikanda katika kubadilishana uzoefu na mbinu bora za kuboresha ujifunzaji wa msingi.

Mkakati wa kuhakikisha kila mtoto anamudu Stadi za KKK katika ngazi za mwanzo unaendana na Dira ya SADC ya kujenga jamii

yenye ujuzi, inayoweza kushiriki kikamilifu katika uchumi wa kikanda na kimataifa.

#### 1.2.2.4 *Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC)*

Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), kupitia Sera yake ya Elimu na Mafunzo na mikakati ya maendeleo ya rasilimali watu, inaweka mkazo katika uimarishaji wa ubora wa elimu na ulinganifu wa viwango vya elimu miongoni mwa nchi wanachama. EAC inatambua kuwa maendeleo ya elimu ya msingi ni sharti la mafanikio ya ajenda ya utangamano wa kikanda, uhamaji wa watu na nguvu kazi yenye ujuzi. Katika mwelekeo huu, EAC inahimiza:

(i) kuimarishwa kwa Elimu ya Awali na msingi ili kujenga msingi imara wa ujifunzaji;

(ii) usawazishaji wa mitaala, viwango vya ujifunzaji na mifumo ya tathmini;

(iii) kukuza matumizi ya lugha zinazotambulika kikanda, ikiwemo Kiswahili, kama nyenzo ya ujifunzaji na mshikamano wa kikanda; na

(iv) ushirikiano wa kikanda katika utafiti, ubunifu na programu za kuboresha ujifunzaji wa msingi.

Mkakati wa kitaifa wa kuhakikisha umahiri wa kumudu Stadi za KKK mwanafunzi afikapo Darasa la Tatu unaenda sambamba na Dira ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC*) ya kujenga rasilimali watu wenye ushindani, jumuishi na inayokidhi mahitaji ya maendeleo ya Afrika Mashariki.

Kwa kuzingatia mwelekeo wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023 na mikakati ya kitaifa, ahadi za kikanda na wajibu wa kimataifa, mkakati huu unajidhihirisha kama chombo muhimu cha kutekeleza maono ya maendeleo ya Tanzania. Mkakati huu hauboreshi ufaulu wa kielimu pekee, bali unaimarisha ustawi wa mtoto kimwili, kiakili na kijamii; unaongeza usawa na ujumuishi katika elimu; na kuweka msingi imara wa ujifunzaji wa maisha yake yote. Kwa kuoanisha juhudi za sekta mbalimbali, kutumia mbinu zilizothibitishwa kama TaRL na kuzingatia matumizi ya takwimu katika kufanya maamuzi, Tanzania inaweza kupunguza kwa kiasi kikubwa ujifunzaji usio na ufanisi, kujenga rasilimali watu wenye ujuzi; na ushindani na kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, Ajenda ya Umoja wa Afrika na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

## 1.3 Uchambuzi wa Uwezo, Udhaifu, Fursa na Changamoto

Mkakati wa Kitaifa wa Kuimarisha Umahiri wa KKK unajengwa juu ya uhalisia wa mfumo wa elimu nchini ili kuhakikisha uchambuzi wa Uwezo, Udhaifu, Fursa na Changamoto umefanyika. Uchambuzi huu unalenga kutambua hali ya halisi ya sasa ya elimu ya awali, kuainisha uwezo uliopo wa Kitaifa, pamoja na kubaini mapungufu ya ndani na vikwazo vya mazingira ya utekelezaji vinavyoathiri ujifunzaji wa Stadi za KKK. Matokeo ya uchambuzi huu yanatumika kama msingi wa kuunda maeneo ya vipaumbele na nguzo za mkakati, kwa lengo la kuhakikisha kuwa afua zinazopendekezwa ni za kimkakati, zinazingatia ushahidi na zinaendana na sera, mipango na muktadha wa maendeleo ya Taifa la Tanzania.

### 1.3.1 Uwezo wa Ndani ya Mfumo

(i) Kuwepo kwa sera, mitaala, mikakati na miongozo ya kitaifa inayotambua umuhimu wa Elimu ya Awali na Stadi za KKK (Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 – Toleo la 2023, Mitaala iliyoboreshwa), Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo (2023-2032), Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Elimu (2025/2026-2029/2030) na Mkakati wa Kitaifa wa Elimu Jumuishi 2021/2022-2025/2026.

(ii) Utashi wa kisiasa na uongozi wa kitaifa unaoonesha dhamira ya dhati ya kuboresha elimu ya msingi, ikiwemo Ilani ya CCM 2025–2030 na msisitizo wa ahadi ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu kuandaa mkakati wa kitaifa wa kisayansi wa KKK ili kuhakikisha kuwa kila mtoto anayeingia Darasa la Tatu anamudu Stadi hizo.

(iii) Kuwepo kwa mtandao wa shule za awali na msingi unaofikia maeneo mengi ya nchi, hivyo kuwezesha utekelezaji wa mkakati kwa kiwango kikubwa.

(iv) Uzoefu uliopo wa walimu katika kufundisha Stadi za KKK, pamoja na programu za mafunzo kazini na Jumuiya za Kujifunza (JzK), ni rasilimali muhimu zinazoweza kuimarishwa zaidi ili kuboresha ubora wa ufundishaji na ujifunzaji.

(v) Kuwepo kwa mifumo ya kitaifa ya taarifa za elimu kama vile BEMIS inayoweza kuboreshwa ili kuhusisha viashiria mahususi vya ujifunzaji wa Stadi za KKK.

### 1.3.2 Udhaifu

(i) Umahiri duni wa walimu katika matumizi ya mbinu shirikishi, tathmini endelevu na ufundishaji unaozingatia viwango halisi vya wanafunzi.

(ii) Upungufu wa walimu wa Darasa la Awali, Darasa la Kwanza na la Pili, pamoja na msongamano wa wanafunzi darasani.

(iii) Matumizi hafifu ya zana na vifaa vya kufundishia, licha ya Kuwepo kwa miongozo na mazingira yanayoweza kutumika.

(iv) Mifumo ya tathmini inayolenga zaidi uandikishaji na mahudhurio badala ya kupima umahiri halisi wa Stadi za KKK.

(v) Matumizi duni ya takwimu katika kupanga na kufanya maamuzi ya kielimu, hasa katika ngazi ya shule hadi taifa.

(vi) Uratibu dhaifu wa utekelezaji wa afua za KKK kati ya ngazi ya Taifa, Mkoa, Halmashauri, Kata na Shule.

(vii) Walimu kutokuwa na utaalamu wa kubainisha wanafunzi wenye mahitaji maalum ya ujifunzaji.

### 1.3.3 Fursa

(i) Ajenda za kikanda na kimataifa (SDGs 2030, AU Education Agenda 2024–2034, SADC, EAC, ADEA, PAL) zinazoweka mkazo kwenye ujifunzaji wa msingi na kupunguza ujifunzaji duni (*learning poverty)*.

(ii) Ushirikiano na wadau wa maendeleo wakiwemo UNICEF, UNESCO, World Bank, WFP wanaovutiwa kuwekeza katika Elimu ya Awali katika Stadi za KKK.

(iii) Ukuaji wa matumizi ya TEHAMA unaowezesha ubunifu katika ufundishaji, tathmini na ufuatiliaji wa KKK.

(iv) Mwamko wa jamii na wazazi/walezi kushiriki katika masuala ya elimu, ikiwemo uchangiaji wa huduma ya chakula shuleni, kuwapa watoto vifaa vya kujifunzia na uboreshaji wa miundombinu.

(v) Kuwepo kwa ushahidi wa kisayansi wa majaribio yaliyothibitishwa mfano. TaRL, *play-based learning* unaoweza kuigwa na kupanuliwa nchini.

(vi) Ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhusu kuandaliwa kwa Mkakati wa Kisayansi wa Stadi za KKK ili kuondoa changamoto ya wanafunzi kutomudu Stadi za KKK wafikapo D arasa la Tatu.

### 1.3.4 Changamoto na Vikwazo vya Nje ya Mfumo

(i) Umaskini wa kaya na mazingira magumu ya maisha huathiri kwa kiasi kikubwa mahudhurio ya watoto shuleni, hali ya lishe, pamoja na utayari wao wa kujifunza.

(ii) Tofauti za kijiografia na kijamii (vijijini, maeneo ya pembezoni, visiwani) zinazoathiri upatikanaji wa rasilimali watu (walimu) na rasilimali vitu.

(iii) Mwamko hasi kwa baadhi ya kaya kuhusu Elimu ya Awali huathiri uandikishaji wa watoto katika elimu ya awali.

(iv) Mitazamo na mila potofu kuhusu Elimu ya Awali katika baadhi ya jamii.

(v) Ufinyu wa bajeti na utegemezi wa rasilimali za nje, yanayoweza kuhatarisha uendelevu wa afua za KKK.

Matokeo ya uchambuzi wa Uwezo, Udhaifu, Fursa na Changamoto yamebainisha kwa uwazi kuwa, pamoja na Kuwepo kwa sera, utashi wa kisiasa na miundombinu ya msingi ya elimu, mfumo wa Elimu ya Awali nchini Tanzania bado unakabiliwa na changamoto za kimuundo na kiutendaji zinazoathiri moja kwa moja ujifunzaji wa Stadi za KKK. Uchambuzi huu pia umeonesha fursa muhimu za kisera, kiteknolojia na kijamii zinazoweza kutumiwa kuharakisha maboresho ya ujifunzaji wa KKK. Kwa kuzingatia matokeo hayo, mkakati huu umejengwa juu ya majibu ya kimkakati yanayolenga kuimarisha uwezo uliopo, kushughulikia mapungufu ya ndani, kutumia fursa zilizopo, na kukabiliana na changamoto za mazingira ya utekelezaji. Hivyo, Nguzo za Mkakati zilizoainishwa hapa chini zinawakilisha maeneo ya kipaumbele ya kitaifa yanayotokana na uchambuzi wa Uwezo, Udhaifu, Fursa na Changamoto, ambazo zitaongoza utekelezaji wa afua zote za kuboresha umahiri wa Stadi za KKK nchini.

## 1.4 Sababu, Mantiki na Uhalali wa Mkakati

Mkakati huu umeandaliwa kutokana na hitaji la kitaifa la kukabiliana na changamoto ya ujifunzaji duni (*learning poverty*) katika Madarasa Elimu ya Awali nchini. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa uzinduzi wa Bunge la 13 tarehe 14 Novemba, 2025 alibainisha masuala mbalimbali ya kipaumbele ambayo yatatakiwa kutekelezwa ndani ya siku 100 za utawala wake. Alisema, "Serikali kuandaa mkakati madhubuti wa kisayansi wa kuhakikisha kila mtoto wa Darasa la Tatu anaweza Kusoma, Kuhesabu na Kuandika bila shida". Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kupanua upatikanaji wa elimu ya msingi, ushahidi wa kitaifa na kimataifa unaonesha kuwa baadhi ya watoto bado hawamudu

Stadi za msingi za KKK wafikapo Darasa la Tatu, hali inarudisha nyuma jitihada za serikali katika kujenga msingi wa ujifunzaji wa baadaye, tija ya rasilimali watu na maendeleo endelevu ya Taifa. Changamoto hii inahitaji mwelekeo mpya unaozingatia ubora wa ujifunzaji, siyo uandikishaji na mahudhurio pekee.

Kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 - Toleo la 2023, Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu (ESDP) 2025/2026–2029/2030, pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2025 – 2030, Serikali imeweka wazi dhamira ya kujenga jamii iliyoelimika, yenye ujuzi na inayoweza kushindana katika uchumi wa kisasa. Hata hivyo, utekelezaji wa dira na sera hizi hauwezi kufikiwa bila kuhakikisha kuwa watoto wanapata misingi imara ya ujifunzaji katika hatua za mwanzo wa elimu. Hivyo, mkakati huu, ni tafsiri ya kisera na kiutendaji ya dhamira ya Taifa ya kuwekeza katika rasilimali watu kwa kuanzia kwenye msingi wa elimu.

Ushahidi wa kisayansi unaonesha kuwa, uwekezaji katika Elimu ya Awali na ujifunzaji wa msingi huleta faida kubwa za kijamii na kiuchumi kuliko uwekezaji katika hatua za baadaye za elimu. Tafiti zinaonesha kuwa, watoto wanaopata elimu bora ya awali, ufundishaji unaomlenga mtoto, walimu mahiri, na afua lengwa za ujifunzaji huonesha maendeleo makubwa katika Stadi za KKK na uwezekano mdogo wa kudondoka shule (Heckman, 2016; World Bank, 2024). Hivyo, mkakati huu umejengwa juu ya mbinu zilizothibitishwa kitaaluma, ikiwemo ujifunzaji kwa michezo, ujifunzaji wa kihisia, tathmini endelevu na ufundishaji unaozingatia kiwango halisi cha mwanafunzi TaRL.

Kwa upande mwingine, uchambuzi wa Uwezo, Udhaifu, Fursa na Changamoto umebainisha kuwa, pamoja na Kuwepo kwa sera, miundombinu ya elimu na utashi wa kisiasa, mfumo wa elimu bado unakabiliwa na idadi ndogo ya walimu ukilinganisha na idadi ya wanafunzi darasani, matumizi hafifu ya takwimu, mapungufu katika mifumo ya uratibu wa afua za KKK, pamoja na changamoto za mazingira ya utekelezaji

kama mwamko hasi kwa baadhi ya kaya kuhusu umuhimu wa Elimu ya Awali na tofauti za kijiografia. Mkakati huu umeundwa mahsusi kushughulikia changamoto hizo kwa kutumia fursa zilizopo za kisera, kiteknolojia na kijamii, na kwa kuimarisha uongozi, uratibu na uendelevu wa utekelezaji.

Mkakati huu pia unaendana na ajenda za kikanda na kimataifa, ikiwemo Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 (hususan SDG 4); Ajenda ya Umoja wa Afrika 2063 na Muongo wa Elimu Afrika (2024–2034); ambazo zinazitaka nchi wanachama kuchukua hatua za haraka kuhakikisha watoto wanamudu Stadi za msingi katika umri unaostahili. Kupitia mkakati huu, Tanzania inatekeleza wajibu wake wa kikanda na kimataifa huku ikijibu mahitaji halisi ya kitaifa.

Kwa misingi hiyo, Mkakati wa Kitaifa wa Kuimarisha Umahiri wa KKK umeandaliwa kama nyenzo ya kisayansi, shirikishi na yenye ushahidi, inayolenga kuunganisha sera, wadau na rasilimali ili kuhakikisha kuwa hakuna mtoto anayevuka Darasa la Pili bila kumudu Stadi za msingi za ujifunzaji. Mkakati huu unatarajiwa kuwa chombo muhimu cha kuimarisha ubora wa elimu, kupunguza pengo la ujifunzaji na kuchangia kwa kiasi kikubwa katika kufikia malengo ya maendeleo ya Taifa kwa muda mfupi, wa kati na mrefu.

## 1.5 Dira na Dhima

### 1.5.1 Dira ya Mkakati

Kuwa na watoto wa Kitanzania wanaomudu Stadi za msingi za KKK katika hatua za mwanzo za elimu, ili kujenga msingi imara wa ujifunzaji katika nyanja zote za maisha na maendeleo endelevu ya Taifa.

### 1.5.2 Dhima ya Mkakati

Kuinua ubora wa ujifunzaji wa Elimu ya Awali kwa kuweka na kutekeleza mifumo madhubuti, shirikishi na bunifu inayotumia TEHAMA na ushahidi wa kitaaluma, itakayowawezesha walimu, wazazi, jamii na wadau wa

elimu kuhakikisha kila mtoto anapata na kumudu Stadi za KKK afikapo Darasa la Tatu.

## 1.6 Malengo, Kanuni, Maadili na Wigo

### 1.6.1 Malengo

#### *1.6.1.1 Lengo Kuu*

Kuhakikisha kila mtoto wa Kitanzania anamudu Stadi za msingi za KKK afikapo Darasa la Tatu kupitia mkakati wa kisayansi, shirikishi na bunifu unaotumia TEHAMA na ushahidi wa kitaaluma

#### *1.6.1.2 Malengo Mahususi*

(i) Kuimarisha Elimu ya Awali kwa ujifunzaji unaomlenga mtoto;

(ii) Kujenga na kuimarisha umahiri wa walimu wa Elimu ya Awali na Darasa la Kwanza na la Pili;

(iii) Kuimarisha mwendelezo wa ujifunzaji katika kipindi mpito kati ya Elimu ya Awali na elimu ya msingi;

(iv) Kuboresha mifumo ya tathmini ya ujifunzaji na utekelezaji wa afua lengwa;

(v) Kuimarisha matumizi ya takwimu, TEHAMA na maamuzi yanayotegemea ushahidi;

(vi) Kuboresha mazingira wezeshi ya ujifunzaji na ustawi wa mtoto; na

(vii) Kuimarisha uongozi, uratibu na uendelevu wa upatikanaji wa rasilimali fedha za utekelezaji wa mkakati.

### 1.6.2 Kanuni Elekezi

**(i) UjifunzajiUnaomlenga Mtoto**

Utekelezaji wa mkakati utaongozwa na kanuni ya kumweka mtoto katika kiini cha ujifunzaji kwa kuzingatia umri, mahitaji Binafsi, uwezo, mazingira ya kijamii na kisaikolojia ya mtoto, ili kuhakikisha ujifunzaji wa Stadi za KKK ni jumuishi, unaovutia na wenye tija.

**(ii) Ujumuishi wa Kielimu**

Mkakati utazingatia kuhakikisha watoto wote, wakiwemo watoto wenye mahitaji maalum wanapata fursa sawa za kujifunza na kumudu Stadi za KKK.

**(iii) Ubora wa Ufundishaji na Umahiri wa Walimu**

Mkakati unatambua kuwa walimu ndio nguzo kuu ya mafanikio ya ujifunzaji wa Stadi za KKK, hivyo utaweka mkazo katika kuimarisha umahiri wao kitaaluma, maadili na matumizi ya mbinu shirikishi, TEHAMA na bunifu katika ufundishaji.

**(iv) Ushahidi wa Kisayansi na Maamuzi Yanaotegemea Takwimu**

Utekelezaji wa mkakati utaongozwa na ushahidi wa kitaaluma, tathmini endelevu na matumizi ya takwimu sahihi za ujifunzaji wa KKK katika kupanga, kufanya maamuzi na kuboresha afua za kielimu.

**(v) Matumizi ya TEHAMA na Ubunifu**

Mkakati utahamasisha matumizi ya TEHAMA na suluhisho bunifu katika ufundishaji, tathmini, ufuatiliaji na ushirikishwaji wa wazazi/walezi na jamii, kwa kuzingatia mazingira na uwezo wa ndani wa nchi.

**(vi) Ushirikiano na Uwajibikaji wa Wadau**

Utekelezaji wa mkakati utategemea ushirikiano wa karibu kati ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, OWM-TAMISEMI, walimu, wazazi, jamii, sekta Binafsi, Asasi za Kiraia (AZAKI) na wadau wa maendeleo, kwa misingi ya uwajibikaji wa pamoja katika kuboresha ujifunzaji wa Stadi za KKK.

**(vii) Mwendelezo wa Ujifunzaji na Uimara wa Mifumo**

Mkakati utazingatia mwendelezo wa ujifunzaji kuanzia Darasa la Awali hadi Darasa la Pili, na kujenga mfumo imara unaoweza kuhimili changamoto za kiuchumi, kijamii na kimazingira.

**(viii) Uendelevu wa Kifedha na Kiutendaji**

Utekelezaji wa mkakati utaongozwa na kanuni ya uendelevu, kwa kuhakikisha rasilimali za kifedha, watu na mifumo zinapatikana, zinasimamiwa na kutumika kwa uwazi na zinaendelezwa kwa muda mrefu.

### 1.6.3 Wigo wa Utekelezaji

Mkakati huu wa Kitaifa wa Kuimarisha Umahiri wa KKK utatumika katika maeneo yote nchini, kwa kuzingatia darasa la elimu ya awali, la Kwanza na la Pili. Wigo wa mkakati unahusisha watoto wanaosoma katika Elimu ya Awali (umri wa miaka 5) na wanafunzi wa Darasa la Kwanza na la Pili katika shule zote za msingi za umma na zisizo za umma.

Kwa upande wa walengwa wa utekelezaji, mkakati huu unawahusisha walimu wa elimu ya awali, walimu wakuu wa shule, wasimamizi wa elimu katika ngazi ya Kata, Halmashauri, Mikoa na Taifa, pamoja na vyuo vya ualimu vinavyohusika na maandalizi ya walimu wa ngazi hizi. Aidha, mkakati unahusisha wazazi, walezi,

jamii, sekta Binafsi, AZAKI na wadau wa maendeleo kama washirika muhimu katika kuimarisha ujifunzaji wa Stadi za KKK.

Kiusimamizi, mkakati huu utatekelezwa chini ya uratibu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na OWM – TAMISEMI, Wizara za kisekta zinazohusika na Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (Afya, Maendeleo ya jamii Jinsia Wanawake na makundi Maalum, Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Maji na Mambo ya Ndani), pamoja na Taasisi za kitaifa za usimamizi, tathmini na takwimu za elimu. Utekelezaji wake utazingatia mgawanyo wa majukumu uliopo katika sera na sheria za elimu nchini.

Kimaudhui, mkakati unahusisha uimarishaji wa ujifunzaji na ufundishaji wa Stadi za KKK, mafunzo ya walimu, tathmini ya ujifunzaji, matumizi ya TEHAMA na takwimu, afua lengwa za wanafunzi wenye changamoto za ujifunzaji, mazingira wezeshi ya ujifunzaji, pamoja na uongozi, uratibu na uendelevu wa kifedha wa afua za Stadi za KKK.

Kwa upande wa muda, mkakati huu utatekelezwa katika kipindi cha miaka mitano 2026/2027–2030/2031, na utaendelea kutumika kama rejea ya kitaifa katika kubuni, kutekeleza na kufuatilia programu na miradi yote inayolenga kuimarisha umahiri wa Stadi za KKK nchini Tanzania.

# 2.0 MPANGO MKAKATI

## 2.1 Nguzo Kuu na Maeneo ya Kimkakati

Mkakati wa Kitaifa wa kuhakikisha kila mtoto anamudu Stadi za KKK umejengwa katika misingi ya ushahidi wa kisayansi, sera za kitaifa na uzoefu wa utekelezaji wa Elimu ya Awali na msingi nchini. Ili kufanikisha utekelezaji wake kwa ufanisi, mkakati huu umegawanywa katika nguzo za kimkakati zinazojikamilisha, ambazo kwa pamoja zinashughulikia masuala ya ujifunzaji wa awali, ufundishaji, tathmini,

mazingira wezeshi, matumizi ya takwimu na uongozi wa utekelezaji. Nguzo hizi zimeandaliwa kwa lengo la kuhakikisha kuwa afua za kuboresha ujifunzaji wa Stadi za KKK zinapangwa, zinatekelezwa na kufuatiliwa kwa mtiririko unaoeleweka na unaolenga matokeo halisi ya ujifunzaji.

### 2.1.1 Elimu ya Awali Jumuishi na Ujifunzaji Unaomlenga Mtoto

Katika muktadha wa Tanzania, Elimu ya Awali imeainishwa katika sera na mipango ya taifa kama msingi wa ujifunzaji na maisha kwa ujumla. Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023 na Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (PJT-MMMAM 2021/2022-2025/2026) zinatambua kuwa wapo watoto wanaingia elimu ya msingi bila misingi imara ya ujifunzaji wa awali, hali inayochangia kushindwa kumudu Stadi za KKK katika madarasa ya mwanzo. Ushahidi wa kimataifa unaunga mkono mtazamo huu kwa kuonesha kuwa watoto wasiopata elimu bora ya ngazi ya awali wako katika hatari kubwa ya ujifunzaji duni afikapo umri wa miaka 10 (Benki ya Dunia, 2022; UNICEF, 2019). Nguzo hii inalenga kuimarisha Elimu ya Awali kwa kutumia mbinu zinazomlenga mtoto, ikiwemo ujifunzaji kwa mbinu ya michezo, ujifunzaji wa kihisia, utambuzi wa mahitaji maalum ya watoto, na ujifunzaji wa KKK nje ya darasa kwa ushirikiano wa wazazi na jamii, ili kuweka msingi imara wa ujifunzaji wa KKK kabla ya mtoto kuingia Darasa la Kwanza.

**Maeneo ya Kimkakati**

(i) Utambuzi wa mapema wa mahitaji ya watoto katika ujifunzaji wa awali.

(ii) Uimarishaji wa ujifunzaji wa Stadi za KKK kwa mbinu ya michezo (*play-based learning*).

(iii) Uimarishaji wa ujifunzaji wa kihisia na kijamii (*Social Emotional Learning – SEL*).

(iv) Uimarishaji wa ujifunzaji wa Stadi za KKK nje ya darasa kwa ushirikiano wa wazazi/walezi na jamii.

(v) Ujumuishaji wa watoto wenye mahitaji maalum katika elimu ya awali.

### 2.1.2 Kuimarisha Uwezo wa Walimu na Mazingira ya Ufundishaji wa Stadi za KKK

Uboreshaji wa ujifunzaji wa Stadi za KKK nchini Tanzania hauwezi kufikiwa bila kuimarisha uwezo wa walimu wa Darasa la Elimu ya Awali la Kwanza na la Pili, ambao ndio watekelezaji wakuu wa mtaala. ESDP 2025/2026–2029/2030 inabainisha kuwa pamoja na kuongezeka kwa uandikishaji wa wanafunzi, changamoto hiyo ya ubora wa ufundishaji bado ipo, hususan katika matumizi ya mbinu shirikishi, zana za kufundishia na kumudu madarasa yenye wanafunzi wengi. Ushahidi wa kisayansi unaonesha kuwa, mafunzo ya awali na endelevu kwa walimu huongeza kwa kiasi kikubwa matokeo ya ujifunzaji wa Stadi za KKK (World Bank, 2018; IPA, 2020). Nguzo hii inalenga kuimarisha; umahiri wa walimu kupitia mafunzo ya kitaaluma, matumizi ya zana na vifaa vya kufundishia, mbinu shirikishi za ufundishaji na ujifunzaji, pamoja na matumizi ya TEHAMA na teknolojia nyingine za kidijitali ili kuhakikisha ufundishaji wa KKK unazingatia mahitaji halisi ya wanafunzi wa Tanzania.

**Maeneo ya Kimkakati**

(i) Maandalizi ya walimu mahiri wa Elimu ya Awali.

(ii) Ajira za walimu wa madarasa ya Elimu ya Awali wenye sifa na mahiri katika Elimu ya Awali.

(iii) Mafunzo ya awali na endelevu kwa walimu wa Darasa la Awali na Darasa la Kwanza na la Pili.

(iv) Uimarishaji wa uwezo wa walimu katika kumudu darasa na kutambua utofauti wa wanafunzi darasani.

(v) Kuimarisha mafunzo katika vyuo vya ualimu ili kuwezesha ufundishaji wa KKK kwa mbinu zilizoboreshwa.

(vi) Shule kuandaa na kutekeleza mkakati wa ufundishaji na uatamizi kwa walimu ambao hawajapata mafunzo ya KKK.

(vii) Uandaaji na matumizi bora ya zana na vifaa vya kufundishia na kujifunzia Stadi za KKK.

(viii) Uimarishaji wa mazingira ya darasa ili yawe rafiki na yenye kuchochea ujifunzaji wa Stadi za KKK.

(ix) Kuimarisha uwezo wa walimu tarajali katika kumudu ufundishaji wa KKK kwa ufanisi.

(x) Matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa Stadi za KKK.

#### 2.1.3 Kuimarisha kipindi cha Mpito Endelevu na Jumuishi katika Ujifunzaji wa Stadi za KKK kutoka Elimu ya Awali hadi Darasa la Kwanza na la Pili

Mabadiliko kutoka Darasa la Awali kwenda Darasa la Kwanza na la Pili ni hatua nyeti katika mfumo wa elimu ya Tanzania. Uzoefu wa utekelezaji wa mitaala ulioboreshwa unaonesha kuwa baadhi ya watoto hukumbana na changamoto za kielimu na kisaikolojia kutokana na tofauti za ghafla za mbinu za ufundishaji na mazingira ya ujifunzaji. Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023 inasisitiza mwendelezo wa ujifunzaji unaomlenga mtoto, wakati ushahidi wa kimataifa unaonesha kuwa vipindi mpito vilivyosimamiwa vizuri huongeza umahiri wa Stadi za msingi (UNESCO, 2021; OECD, 2019). Nguzo hii inalenga kuimarisha uoanifu wa mitaala, mbinu na mazingira ya ujifunzaji, pamoja na ushirikiano wa

walimu wa Elimu ya Awali na wa Darasa la Kwanza na la Pili, ili kuhakikisha watoto wanapita katika ngazi hizi kwa ufanisi na kuendelea kumudu Stadi za KKK.

**Maeneo ya Kimkakati**

(i) Uoanifu wa mitaala na matarajio ya ujifunzaji kati ya Darasa la Awali, Darasa la Kwanza na la Pili.

(ii) Uimarishaji wa mazingira rafiki ya ujifunzaji katika Darasa la Awali, la Kwanza na la Pili.

(iii) Ushirikiano wa kitaaluma kati ya walimu wa Darasa la Awali, la Kwanza na la Pili.

(iv) Maandalizi ya mtoto kisaikolojia na kijamii kwa kipindi cha mpito.

(v) Ufuatiliaji wa maendeleo ya ujifunzaji wa Stadi za KKK katika kipindi cha mpito.

### 2.1.4 Kuimarisha Tathmini ya Ujifunzaji na Afua za Kurekebisha Ujifunzaji wa Stadi za KKK)

Changamoto ya ujifunzaji duni nchini Tanzania inahitaji mfumo wa tathmini unaozingatia matokeo halisi ya ujifunzaji kuliko uandikishaji na mahudhurio pekee. ESDP 2025/2026–2029/2030 inasisitiza matumizi ya tathmini endelevu ili kubaini mapema changamoto za ujifunzaji. Ushahidi wa kimataifa unaonesha kuwa mbinu ya *TaRL* imefanikiwa kuongeza uwezo wa KKK kwa wanafunzi katika nchi nyingi zenye mazingira yanayofanana na Tanzania (J-PAL, 2019; World Bank, 2022). Nguzo hii inalenga kuimarisha tathmini za ujifunzaji na utekelezaji wa afua lengwa ili kuhakikisha kila mtoto anafundishwa kulingana na kiwango chake halisi cha uelewa na kupunguza ujifunzaji duni katika madarasa ya mwanzo.

**Maeneo ya Kimkakati**

(i) Uimarishaji wa tathmini endelevu ya ujifunzaji wa Stadi za KKK katika madarasa ya awali.

(ii) Utambuzi wa mapema wa wanafunzi wenye changamoto za ujifunzaji wa Stadi za KKK.

(i) Utekelezaji wa mbinu ya *TaRL* na afua zingine lengwa.

(iii) Uimarishaji wa madarasa mbadala na programu za kurekebisha ujifunzaji (catch-up programmes).

(iv) Matumizi ya matokeo ya tathmini katika kuboresha ufundishaji na kupanga afua.

### 2.1.5 Kuimarisha Mifumo ya Takwimu, TEHAMA na Maamuzi Yanayotokana na Ushahidi katika Ujifunzaji wa Stadi za KKK

Serikali ya Tanzania imeendelea kuimarisha matumizi ya takwimu katika kupanga na kufuatilia maendeleo ya sekta ya elimu kupitia mifumo ya kielimu kama BEMIS - SIS. Hata hivyo, ripoti za kitaifa na kimataifa zinaonesha kuwa, bado kuna hitaji la kuimarisha matumizi ya takwimu zinazopima matokeo halisi ya ujifunzaji wa KKK (World Bank, 2020; UNESCO, 2022). Nguzo hii inalenga kuimarisha mifumo ya takwimu na TEHAMA ili kuwezesha ukusanyaji, uchambuzi na matumizi ya taarifa za ujifunzaji wa Stadi za KKK katika kufanya maamuzi ya kisera, kuboresha ufundishaji na kuongeza uwajibikaji katika ngazi zote.

**Maeneo ya Kimkakati**

(i) Uimarishaji wa mifumo ya ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu za ujifunzaji wa Stadi za KKK.

(ii) Matumizi ya mifumo ya kidijitali (BEMIS-SIS) na mifumo mingine katika ufuatiliaji wa Stadi za KKK.

(iii) Kuanzishwa na kutumia Dashibodi ya Taifa ya Stadi za KKK.

(iv) Kujenga uwezo wa watendaji wa elimu katika matumizi ya takwimu na TEHAMA.

(i) Kufanya tafiti za kitaaluma na kutoa mrejesho wa tafiti hizo kwa shule, jamii na watunga sera.

### 2.1.6 Kuimarisha Ustawi, Ulinzi na Mazingira Wezeshi ya Ujifunzaji kwa Watoto wa Elimu ya Awali na Darasa ya la Kwanza na la Pili

Katika mazingira ya Tanzania, masuala ya chakula shuleni, miundombinu, zana/vifaa vya kujifunzia na kufundishia, usalama na ulinzi wa mtoto, na ushiriki wa wazazi/walezi yana mchango mkubwa katika ujifunzaji wa watoto. Ripoti za FAO (2019) na WFP (2020; 2024) zinaonesha kuwa, huduma ya chakula shuleni huongeza uandikishaji, mahudhurio, umakini na ufaulu wa wanafunzi. Nguzo hii inalenga kuimarisha mazingira wezeshi ya ujifunzaji kwa kuzingatia ustawi wa mtoto, ikiwemo lishe, miundombinu rafiki, mazingira salama na ushiriki wa wazazi na jamii, kama msingi wa kufanikisha ujifunzaji wa KKK.

**Maeneo ya Kimkakati**

(i) Upatikanaji wa huduma ya chakula na lishe shuleni.

(ii) Uimarishaji wa miundombinu rafiki kwa watoto wa Darasa la Elimu ya Awali, la Kwanza na la Pili.

(iii) Uhakika wa mazingira salama, jumuishi na yenye ulinzi kwa mtoto.

(iv) Ushirikiano wa wazazi/walezi na jamii katika ustawi na ujifunzaji wa watoto.

(v) Upatikanaji wa huduma za msingi (maji, vyoo, Afya) katika shule.

### 2.1.7 Kuimarisha Uongozi, Uratibu, Ufadhili Endelevu na Uwajibikaji katika Utekelezaji wa Mkakati wa Stadi za KKK

Utekelezaji wa mkakati wa Stadi za KKK unahitaji uongozi thabiti, uratibu wa Taasisi na uendelevu wa rasilimali za kifedha. Ilani ya CCM 2025–2030 na ESDP 2025/2026–2029/2030 zinaweka mkazo katika uwekezaji endelevu katika elimu bora na uwajibikaji wa utekelezaji. Ushahidi wa imataifa unaonesha kuwa mikakati ya elimu inayofanikiwa hutegemea mifumo madhubuti ya uongozi, uratibu na ufuatiliaji (UNESCO-GEM, 2020; 2023).

Changamoto za ujifunzaji duni wa Stadi za KKK haziwezi kushughulikiwa ipasavyo bila ushirikiano kati ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, OWM-TAMISEMI, shule, walimu, wazazi/walezi, jamii na wadau wa Maendeleo. Nguzo hii inalenga kuimarisha mifumo ya uongozi na uratibu, kukuza ushirikiano wa wadau, pamoja na kupanga na kusimamia rasilimali kwa ufanisi ili kuhakikisha utekelezaji wa mkakati huu. Kupitia nguzo hii, mkakati utaweza kutekelezwa kwa uwajibikaji, kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara na endelevu ili kuleta matokeo chanya na ya kudumu katika ujifunzaji wa Stadi za KKK nchini. Aidha, Mkakati utaweka wazi majukumu ya kila mdau kama yatakavyofafanuliwa katika Mwongozo utakaoandaliwa kwa lengo la kufanikisha Mkakati huu kwa wakati muafaka. Katika kufanya hivyo, mwongozo utabainisha majukumu kwa kuzingatia vigezo maalumu vikiwemo majukumu ya kimfumo, Kisera na kiutendaji. Sambamba na hilo, mwongozo utaweka wazi suala zima la uratibu katika ngazi zote za elimu, Kitaifa (Wizara), Kikanda, Mikoa na Halmashauri.

**Maeneo ya Kimkakati**

(i) Uongozi na uratibu wa kitaifa wa utekelezaji wa mkakati wa Stadi za KKK.

(ii) Uratibu wa sekta mtambuka (WyEST, OWM-TAMISEMI, Wizara ya Afya, Wizara ya Fedha n.k.).

(iii) Uendelevu wa kifedha kupitia bajeti maalum ya mafunzo ya Stadi za KKK na ubia wa wadau.

(iv) Ufuatiliaji, tathmini na uwajibikaji wa utekelezaji wa mkakati.

(v) Ushirikiano na wadau wa maendeleo, AZAKI na sekta Binafsi.

## 3.0 BANGO KITITA LA MKAKATI WA KISAYANSI WA KUIMARISHA STADI ZA KKK

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Elimu ya Awali Jumuishi na Ujifunzaji Unaomlenga Mtoto | **1.1: Utambuzi wa Mahitaji Maalum ya Watoto katika Ujifunzaji wa Awali** | Kuandaa mwongozo wa kitaifa wa utambuzi wa mapema wa mahitaji ya ujifunzaji kwa watoto wa Elimu ya Awali ifikapo Desemba 2026. | Kuwepo kwa Kuwepo kwa Mwongozo wa utambuzi wa Sifa. | 80,000,000.00 | Januari 2026 - Desemba 2026 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Wizara yenye dhamana na Maendeleo ya Jamii. |
| | | | Kuwajengea uwezo walimu wa Darasa la Awali na Darasa la I–II katika kubaini changamoto za ujifunzaji wa KKK mapema ifikapo Desemba 2028. | Idadi na asilimia ya walimu wa Darasa la Awali na I–II waliopata mafunzo maalum ya utambuzi wa changamoto za KKK. | 91,822,950,000.00 | Juni 2026-Desemba 2028 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Wizara yenye dhamana ya Afya, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Sekta Binafsi, Wadau wa Maendeleo. |
| | | | Kuandaa utaratibu wa kufuatilia maendeleo ya watoto wenye mahitaji maalum ya ujifunzaji katika ngazi ya shule Ifikapo Juni 2027. | Mwongozo/utaratibu rasmi wa shule wa ufuatiliaji wa maendeleo ya watoto wenye mahitaji maalum umeandaliwa na kuanza kutumika | 80,000,000.00 | Juni 2026-Juni 2027 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Wizara yenye dhamana ya Maendeleo ya Jamii, Sekta Binafsi. |
| | | | Kushirikisha wazazi na walezi katika kubaini, kutoa taarifa na kufuatilia mahitaji ya ujifunzaji ya watoto | Kuwepo kwa utaratibu rasmi wa mawasiliano kati ya shule na wazazi/walezi | 0.00 | Julai 2026-Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa. |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | wao Ifikapo Juni 2030. | (daftari la mawasiliano, simu, ujumbe. | | | |
| | | **1.2: Kuimarisha Ujifunzaji kwa Njia ya Michezo (Play-Based Learning)** | Kuandaa na kusambaza mwongozo wa kitaifa wa ujifunzaji wa KKK kwa njia ya michezo ifikapo Juni 2027. | Kuwepo kwa Kuwepo kwa Mwongozo wa kitaifa wa ujifunzaji wa KKK kwa njia ya michezo. | 80,000,000.00 | Juni 2026-Juni 2027 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Wizara yenye dhamana na michezo, Sekta Binafsi, Wadau wa Maendeleo. |
| | | | Kuwajengea uwezo walimu wa Elimu ya Awali na madarasa ya chini kutumia michezo kama mbinu ya kufundishia KKK, Kuanzisha na kuimarisha kona za michezo na ujifunzaji katika madarasa ya Elimu ya Awali ifikapo Juni 2027. | Kuimarika kwa Stadi za KKK kwa watoto wanaofundishwa kwa kutumia michezo. | 91,822,950,000.00 | Julai 2026-Juni 2027 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Sekta Binafsi, Taasisi za Elimu, Wadau wa Maendeleo. |
| | | | Kuhamasisha matumizi ya michezo iliyopo katika mazingira halisi ya mtoto na jamii yake katika kujifunza KKK ifikapo Juni 2030. | Watoto kushiriki kikamilifu michezo ya jadi/kijamii. | 79,400,000.00 | Januari 2026-Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Sekta Binafsi, Taasisi za |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | Elimu, Wadau wa Maendeleo. |
| | | | Kutumia mbinu za michezo katika tathmini na ufundishaji wa Stadi za KKK darasani ifikapo Juni 2030. | Kuongezeka kwa umahiri wa wanafunzi katika kumudu Stadi za KKK. | 0.00 | Januari 2026-Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi za Elimu, Wadau wa Maendeleo. |
| | | **1.3: Kuimarisha Ujifunzaji wa Kihisia na Kijamii (Social Emotional Learning – SEL)** | Kuandaa Mwongozo wa Kitaifa wa Ujifunzaji wa Kihisia na Kijamii (*SEL*) kwa Elimu ya Awali ifikapo Juni 2027. | Kuwepo kwa Mwongozo wa Kitaifa wa Ujifunzaji wa Kihisia na Kijamii (*SEL*). | 80,000,000.00 | Julai 2026-Juni 2027 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya Afya, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI. |
| | | | Kuwajengea uwezo walimu wa Elimu ya Awali katika kufundisha Stadi za kujitambua, kudhibiti hisia, kushirikiana na kujiamini ifikapo Juni 2027. | Idadi/Asilimia ya walimu wa Elimu ya Awali waliopata mafunzo. | 9,822,950,000.00 | Julai 2026-Juni 2027 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Sekta Binafsi, Wadau wa Maendeleo. |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kuingiza vipengele vya ujifunzaji wa kihisia katika shughuli za kila siku za darasa na michezo ya watoto ifikapo Juni 2027. | Idadi/Asilimia ya madarasa ya Elimu ya Awali yanayotumia kwa uthabiti vipengele vya ujifunzaji wa kihisia (SEL). | 0.00 | Julai 2026-Juni 2027 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Sekta Binafsi, Wadau wa Maendeleo. |
| | | | Kuandaa na kutumia nyenzo rahisi zitakazosaidia watoto kukuza ustahimilivu wa kihisia na mahusiano chanya ifikapo Juni 2027. | Idadi/Asilimia ya vituo vya Elimu ya Awali vinavyoandaa na kutumia kikamilifu nyenzo rahisi, rafiki kwa mtoto. | 0.00 | Julai 2026-Juni 2027 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Sekta Binafsi Wadau wa Maendeleo. |
| | | | Kuelimisha wazazi na jamii kuhusu umuhimu wa SEL katika kujenga msingi wa ujifunzaji wa Stadi za KKK ifikapo Juni 2027. | Asilimia ya wazazi na wanajamii walioelimishwa au kushiriki katika shughuli za SEL. | 75,000,000.00 | Julai 2026-Juni 2027 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Sekta Binafsi, Wadau wa Maendeleo. |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **1.4: Kuimarisha Ujifunzaji wa Stadi za KKK Nje ya Darasa** | Kuandaa mwongozo wa kitaifa wa ujifunzaji wa Stadi za KKK nje ya darasa kwa watoto wa Elimu ya Awali ifikapo Juni 2028. | Kuwepo kwa Mwongozo wa kitaifa wa ujifunzaji wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) nje ya darasa umeandaliwa. | 80,000,000.00 | Julai 2027-Juni 2028 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Sekta Binafsi, Wadau wa Maendeleo. |
| | | | Kuwajengea uwezo walimu kuunganisha ujifunzaji wa darasani na shughuli za ujifunzaji nje ya darasa ifikapo Juni 2028. | Idadi/Asilimia ya walimu wa Elimu ya Awali waliopatiwa mafunzo. | 91,822,950,000.00 | Julai 2027-Juni 2028 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Wadau wa Maendeleo. |
| | | | Kuelimisha wazazi na walezi kuhusu mbinu rahisi za kusaidia watoto kujifunza Stadi za KKK nyumbani ifikapo Juni 2028. | Idadi na asilimia ya wazazi na walezi walioelimishwa. | 0.00 | Julai 2027-Juni 2028 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Wadau wa Maendeleo. |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kukuza matumizi ya mazingira ya jamii kama rasilimali za kujifunzia Stadi za KKK, ikiwemo soko, shamba, nyumbani na maeneo ya kijamii ifikapo Juni 2028. | Idadi/Asilimia ya walimu na madarasa ya Elimu ya Awali yanayotumia kwa uthabiti mazingira ya jamii. | 0.00 | Julai 2027-Juni 2028 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Wadau wa Maendeleo. |
| | | | Kufuatilia mchango wa ujifunzaji nje ya darasa katika maendeleo ya umahiri wa Stadi za KKK kwa watoto ifikapo Juni 2030. | Idadi/ Asilimia ya watoto walioonyesha maendeleo chanya katika Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK). | 74,000,000.00 | Julai 2026-Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu, Wadau wa Maendeleo. |
| | | **1.5: Ushirikiano wa Wazazi na Jamii katika Elimu ya Awali** | Kuimarisha utekelezaji wa mwongozo wa Ushirikiano wa Walimu na Wazazi (UWaWa) katika shule za Elimu ya Awali ifikapo Juni 2029. | Asilimia ya shule za Elimu ya Awali zinazotekeleza mwongozo wa UWaWa kikamilifu. | 0.00 | Julai 2028-Juni 2029 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana Maendeleo ya Jamii na Makundi Maalumu. |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kuandaa na kuendesha vikao vya nusu mwaka vya wazazi na walimu kwa ajili ya kujadili na kufuatilia maendeleo ya ujifunzaji wa Stadi za KKK kwa watoto ifikapo Juni 2029. | Idadi/Asilimia ya vikao vya wazazi na walimu vinavyofanyika. | 0.00 | Julai 2028-Juni 2029 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Wizara yenye dhamana na Maendeleo ya Jamii. |
| | | | Kushirikisha jamii katika kuboresha mazingira ya ujifunzaji wa Elimu ya Awali, ikiwemo miundombinu na usalama wa watoto ifikapo Juni 2029. | Idadi/Asilimia ya shule za Elimu ya Awali zinazoshirikisha jamii. | 0.00 | Julai 2028-Juni 2029 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Wizara yenye dhamana ya Maendeleo ya Jamii, Wadau wa Maendeleo. |
| | | | Kuhamasisha jamii kulinda haki, usalama na ustawi wa watoto kama msingi wa ujifunzaji bora ifikapo Juni 2029. | Asilimia ya wazazi, walezi, na wanajamii waliopatiwa elimu au kushiriki. | 0.00 | Julai 2028-Juni 2029 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Wizara yenye dhamana na Maendeleo ya Jamii. |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kutumia viongozi wa jamii na dini kama mabalozi wa kuhamasisha ujifunzaji wa Stadi za KKK katika jamii ifikapo Juni 2029. | Asilimia ya viongozi wa jamii na dini walioshiriki. | 0.00 | Julai 2028-Juni 2029 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Viongozi wa dini, Wadau wa Maendeleo. |
| **Mahitaji ya Fedha kufikia Lengo** | | | | | **367,920,200,000.00** | | |
| 2. | **Umahiri wa Walimu na Ubora wa Ufundishaji wa KKK** | **2.1: Mafunzo ya Awali na Endelevu kwa Walimu wa Elimu ya Awali** | Kuandaa mpango wa kitaifa wa mafunzo endelevu (MEWAKA) kwa walimu wa Darasa la awali na Darasa la I–II unaolenga umahiri wa Stadi za KKK ifikapo Juni 2029. | Kuwepo kwa Mpango wa Kitaifa wa Mafunzo Endelevu (MEWATA). | 80,000,000.00 | Julai 2028-Juni 2029 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taaisi za Elimu, Sekta Binafsi, Wadau wa Maendeleo. |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kurekebisha na kuoanisha maudhui ya mafunzo ya walimu katika vyuo vya ualimu ili yaendane na mbinu za kisasa za ufundishaji wa Stadi za KKK ifikapo Juni 2029 | Asilimia ya programu za mafunzo ya walimu katika vyuo vya ualimu zilizorekebishwa na kuoanisha maudhui yake ili ziwe sambamba na mbinu za kisasa za kufundisha Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK). | 50,000,000.00 | Julai 2028-Juni 2029 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu, Wadau wa Maendeleo. |
| | | | Kutoa mafunzo kwa walimu kuhusu ufundishaji wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu kwa kuzingatia maendeleo ya mtoto ifikapo Juni 2029. | Asilimia ya walimu wa Elimu ya Awali na Darasa la I–II waliohudhuria mafunzo ya mara kwa mara yanayolenga mbinu za kufundisha Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa kuzingatia maendeleo ya mtoto. | 91,822,950,000.00 | Julai 2028-Juni 2029 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kuandaa na kusambaza miongozo ya kitaaluma kwa walimu kuhusu ufundishaji bora wa Stadi za KKK ifikapo Juni 2029. | Idadi/Asilimia ya miongozo ya kitaaluma kuhusu ufundishaji bora wa Stadi za KKK iliyoandaliwa na kusambazwa. | 80,000,000.00 | Julai 2028-Juni 2029 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |
| | | | Kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji wa matokeo ya mafunzo ya walimu katika kuboresha ujifunzaji wa Stadi za KKK ifikapo Juni 2029. | Asilimia ya shule au Taasisi za Elimu zinazotekeleza mifumo. | 0.00 | Julai 2028-Juni 2029 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |
| | | **2.2: Kuimarisha Umahiri wa Walimu katika Kumudu Darasa na Tofauti za Wanafunzi** | Kuwajengea uwezo walimu katika mbinu za kumudu madarasa yenye wanafunzi wengi na wenye viwango tofauti vya ujifunzaji ifikapo Juni 2029. | Idadi/Asilimia ya walimu waliopewa mafunzo katika mbinu za kumudu madarasa yenye wanafunzi wengi na viwango tofauti vya ujifunzaji. | 91,822,950,000.00 | Julai 2028-Juni 2029 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Wadau wa Maendeleo. |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kutoa mafunzo kuhusu utambuzi wa mahitaji ya kila mwanafunzi na utoaji wa afua stahiki darasani ifikapo Juni 2029. | Asilimia ya walimu waliohudhuria mafunzo. | 0.00 | Julai 2028-Juni 2029 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |
| | | | Kuimarisha matumizi ya mbinu shirikishi zinazowezesha ushiriki wa wanafunzi wote katika ujifunzaji wa Stadi za KKK ifikapo Juni 2029. | Idadi/Asilimia ya walimu wanaotumia mbinu shirikishi darasani. | 0.00 | Julai 2028-Juni 2029 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Sekta Binafsi. |
| | | | Kuwajengea walimu uwezo wa kuandaa mazingira rafiki, salama na jumuishi ya Darasa la Elimu ya Awali na Darasa la I na la II ifikapo Juni 2029. | Idadi/Asilimia ya walimu waliopewa mafunzo. | 91,822,950,000.00 | Julai 2028-Juni 2029 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Sekta Binafsi. |
| | | | Kuimarisha mahusiano chanya kati ya walimu na wanafunzi ili kuongeza | Idadi/Asilimia ya walimu wanaoonesha uhusiano chanya | 0.00 | Julai 2028-Juni 2029 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM- |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | ari na motisha ya kujifunza ifikapo Juni 2029. | na wanaowaelewa wanafunzi wao. | | | TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Sekta Binafsi. |
| | | **2.3: Uandaaji na Matumizi ya Zana na Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia Stadi za KKK** | Kuandaa mwongozo wa kitaifa wa uandaaji na matumizi ya zana na vifaa vya kufundishia wa Stadi za KKK kwa kutumia rasilimali za mazingira ya shule na jamii ifikapo Juni 2029. | Kuwepo kwa Mwongozo wa Kitaifa | 80,000,000.00 | Julai 2028-Juni 2029 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Sekta Binafsi, Wadau wa Maendeleo. |
| | | | Kuwajengea uwezo walimu wa kubuni, kutengeneza na kutumia zana rahisi na bunifu za kufundishia Stadi za KKK ifikapo Juni 2029. | Idadi/Asilimia ya walimu waliopata mafunzo. | 0.00 | Julai 2028-Juni 2029 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Sekta Binafsi, wadau wa maendeleo |
| | | | Kuhamasisha ufaraguzi wa zana halisi katika ufundishaji wa Stadi za KKK ifikapo Juni 2029. | Idadi/Asilimia ya walimu wanaotumia kwa uthabiti zana halisi. | 0.00 | Julai 2028-Juni 2029 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | dhamana ya Teknolojia, Sekta Binafsi, Wadau wa Maendeleo. |
| | | | Kuimarisha matumizi ya Jumuiya za Kujifunzia (JzK) kama jukwaa la kubadilishana uzoefu wa matumizi ya zana ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya walimu wanaoshiriki kikamilifu katika Jumuiya za Kujifunzia (JzK). | 50,000,000.00 | Julai 2028-Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Sekta Binafsi, Wadau wa Maendeleo. |
| | | | Kufuatilia na kutathmini matumizi ya zana na vifaa katika ufundishaji wa Stadi za KKK darasani ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya madarasa au walimu wanaofuatiliwa na kutathminiwa. | 90,000,000.00 | Julai 2028-Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Sekta Binafsi, Wadau wa Maendeleo. |
| | | **2.4: Kuimarisha Usimamizi na Ufuatiliaji wa Kitaaluma Shuleni** | Kuimarisha uwezo wa Walimu Wakuu na Wathibiti Ubora wa Shule katika kusimamia ufundishaji wa Stadi za KKK kwa mtazamo wa kitaaluma kwa kutumia | Idadi/Asilimia ya Walimu wakuu na Wathibiti Ubora wa Shule waliopewa mafunzo. | 91,822,950,000.00 | Julai 2027-Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | mifumo ya TEHAMA ifikapo Juni 2030. | | | | Teknolojia, Sekta Binafsi, Wadau wa Maendeleo. |
| | | | Kuandaa na kutumia zana za ufuatiliaji wa ubora wa ufundishaji wa Stadi za KKK shuleni ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya shule zinazotumia zana zilizoundwa za ufuatiliaji wa ubora wa ufundishaji wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK). | 28,400,000.00 | Julai 2027-Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Sekta Binafsi, Wadau wa Maendeleo. |
| | | | Kuweka utaratibu wa uatamizi na usaidizi (mentorship and coaching) kwa walimu wa madarasa ya Elimu ya Awali na Darasa la I - II ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya walimu wa Elimu ya Awali na Darasa la I–II wanaopokea uatamizi na usaidizi wa kitaaluma (Mentorship na Coaching). | 2,712,600,000.00 | Julai 2027-Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Sekta Binafsi, Wadau wa Maendeleo. |
| | | | Kutumia matokeo ya ufuatiliaji wa kitaaluma ili kuboresha mafunzo na kutoa afua stahiki kwa walimu ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya walimu wanaopokea mafunzo na afua stahiki. | 0.00 | Julai 2027 - Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Sekta |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | Binafsi, Wadau wa Maendeleo. |
| | | **2.5: Matumizi ya TEHAMA na Ubunifu katika Ufundishaji wa Stadi za KKK** | Kuwajengea uwezo walimu kutumia TEHAMA na teknolojia nyingine za kufundishia na kujifunzia kama nyenzo ya ufundishaji na ujifunzaji wa Stadi za KKK kulingana na mazingira ya shule ifikapo Juni 2028. | Idadi/Asilimia ya walimu waliopewa mafunzo. | 91,822,950,000.00 | Julai 2027 - Juni 2028 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Sekta Binafsi, Wadau wa Maendeleo. |
| | | | Kuandaa na kusambaza nyenzo za kidijitali za ufundishaji wa Stadi za KKK (maudhui ya sauti, picha na video) ifikapo Juni 2028. | Idadi/Asilimia ya shule au walimu waliopewa na kutumia nyenzo za kidijitali zilizoundwa. | 52,000,000.00 | Julai 2027-Juni 2028 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Sekta Binafsi, Wadau wa Maendeleo. |
| | | | Kukuza matumizi ya teknolojia rahisi (redio, simu janja, vishikwambi, vifaa vya nje ya mtandao) katika ufundishaji wa Stadi za KKK ifikapo Juni | Idadi/Asilimia ya walimu au shule zinazotumia teknolojia rahisi. | 34,250,000,000.00 | Julai 2027 - Juni 2028 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2028. | | | | dhamana ya Teknolojia, Sekta Binafsi, Wadau wa Maendeleo. |
| | | | Kuhamasisha ubunifu wa walimu katika kutumia TEHAMA na teknolojia nyingine za kufundishia na kujifunzia ili kuboresha ujifunzaji wa Stadi za KKK ifikapo Juni 2028. | Idadi/Asilimia ya walimu wanaotumia TEHAMA na mbinu nyingine bunifu za kufundishia na kujifunzia. | 0.00 | Julai 2027-Juni 2028 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Sekta Binafsi, Wadau wa Maendeleo. |
| | | | Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya mchango wa TEHAMA na teknolojia nyingine katika kuboresha umahiri wa Stadi za KKK ifikapo Juni 2028. | Idadi/Asilimia ya shule au walimu wanaofuatiliwa na kutathminiwa. | 126,000,000.00 | Julai 2027-Juni 2028 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Sekta Binafsi, Wadau wa Maendeleo. |
| **Mahitaji ya Fedha kufikia Lengo** | | | | | **496 713 750 000.00** | | |
| 3. | **Kuimarisha Mwendelezo wa Ujifunzaji Kipindi cha Mpito kati ya Darasa la** | **3.1: Mwendelezo wa Mtaala, Mbinu na Matarajio ya Ujifunzaji** | Kuandaa utaratibu utakaotoa maelekezo kuhusu kipindi cha mpito cha ujifunzaji wa Stadi za KKK kati ya Darasa la Elimu ya | Idadi/Asilimia ya shule zinazotekeleza utaratibu wa kitaifa unaoelekeza namna ya | 44,000,000,000.00 | Julai 2026-Juni 2027 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Elimu ya Awali na Darasa la I-II** | | Awali, Darasa la I- II ifikapo Juni 2027. | kusimamia kipindi mpito cha ujifunzaji wa KKK. | | | Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |
| | | | Kuoanisha mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazotumika katika Darasa la Elimu ya Awali na Darasa la I–II, kwa kuzingatia mtaala uliohoreshwa ifikapo Juni 2027. | Idadi/Asilimia ya walimu wanaoendesha ufundishaji kwa kutumia mbinu zinazooanishwa. | 0.00 | Julai 2026 - Juni 2027 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |
| | | | Kuhakikisha matumizi endelevu ya mbinu za ujifunzaji kwa michezo na shughuli katika Darasa la Kwanza na la Pili ifikapo Juni 2027. | Idadi/Asilimia ya walimu wa Darasa la Kwanza na la Pili wanaofundisha kwa kutumia mbinu ya michezo. | 0.00 | Julai 2026 - Juni 2027 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |
| | | | Kutoa maelekezo ya kitaaluma kuhusu matarajio ya umahiri wa Stadi za KKK kwa kila ngazi ya Darasa la Awali hadi Darasa la Pili ifikapo Juni 2027. | Idadi/Asilimia ya walimu au shule zinazopokea na kutumia maelekezo. | 0.00 | Julai 2026 - Juni 2027 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kufuatilia utekelezaji wa mwendelezo wa mtaala katika shule za msingi ifikapo Juni 2027. | Idadi/Asilimia ya shule za msingi zinazofuatilia, kutathmini na kuripoti utekelezaji. | 74,000,000,00 | Julai 2026 - Juni 2027 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |
| | | **3.2: Uratibu wa Kitaaluma kati ya Walimu wa Elimu ya Awali** | Kuanzisha utaratibu wa vikao vya pamoja vya kitaaluma ili kubadilishana uzoefu na mbinu bora za ufundishaji wa Stadi za KKK kati ya walimu wa Darasa la Awali na walimu wa Darasa la I–II ifikapo Juni 2028. | Idadi/Asilimia ya shule zinazoendesha vikao vya pamoja. | 0.00 | Julai 2027 - Juni 2028 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |
| | | | Kuweka mfumo wa uatamizi (mentorship) kati ya walimu wa Darasa la Awali na walimu wa Darasa la I–II ifikapo Juni 2028. | Idadi/Asilimia ya shule zinazotekeleza mfumo wa uatamizi kati ya walimu wa Darasa la Awali na walimu wa Darasa la I–II. | 0.00 | Julai 2027- Juni 2028 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kuchopeka ratiba za vikao vya walimu wa madarasa ya Elimu ya Awali katika utaratiba wa shule ifikapo Juni 2028. | Idadi/Asilimia ya shule zinazopanga na kuingiza vikao. | 0.00 | Julai 2027-Juni 2028 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |
| | | | Kufuatilia mchango wa uratibu wa walimu katika kuboresha ujifunzaji wa Stadi za KKK ifikapo Juni 2028. | Idadi/Asilimia ya shule zinazofuatiliwa ambazo uratibu wa walimu unaonyesha mchango chanya. | 74,000,000.00 | Julai 2027-Juni 2028 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |
| | | **3.3: Uimarishaji wa Mazingira Rafiki ya Kipindi cha Mpito** | Kuboresha muonekano wa Darasa la Awali, Darasa la Kwanza na la Pili ili yaendane na mazingira ya Elimu ya Awali ifikapo Juni 2028. | Idadi/Asilimia ya madarasa ya Darasa la Kwanza na la Pili yaliyoboreshwa ili kuendana na mahitaji ya wanafunzi. | 2,312,500,000.00 | Julai 2027-Juni 2028 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Wizara yenye dhamana ya Mazingira, Taasisi za Elimu. |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kuanzisha na kuimarisha kona za ujifunzaji na vifaa shirikishi katika Madarasa ya Awali, I - II ifikapo Juni 2028. | Idadi/Asilimia ya madarasa ya Awali hadi Darasa la III yaliyoanzisha na kuimarisha kona za ujifunzaji. | 0.00 | Julai 2027-Juni 2028 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |
| | | | Kuhakikisha mazingira salama, jumuishi na yanayozingatia mahitaji ya kijinsia na watoto wenye mahitaji maalum ifikapo Juni 2028. | Idadi/Asilimia ya shule zenye madarasa yaliyoandaliwa na kudumishwa. | 0.00 | Julai 2027-Juni 2028 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |
| | | | Kuimarisha huduma za ustawi wa mtoto katika kipindi cha mpito, ikiwemo usafi, Afya, ulinzi na usalama ifikapo Juni 2028. | Idadi/Asilimia ya shule zinazotoa huduma za ustawi wa mtoto zinazoimarisha usafi, Afya, ulinzi na usalama. | 0.00 | Julai 2027-Juni 2028 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kufuatilia ubora wa mazingira ya ujifunzaji katika kipindi cha mpito ifikapo Juni 2028. | Idadi/Asilimia ya shule zinazofuatiliwa | 74,000,000.00 | Julai 2027-Juni 2028 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |
| | | | Kufuatilia maendeleo ya watoto katika kipindi cha mpito ili kutoa afua stahiki mapema ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya watoto waliofuatiliwa na kutathminiwa | 74,000,000.00 | Julai 2027-Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |
| | | **3.4: Utayari wa Mtoto Kisaikolojia, Kijamii na Kielimu** | Kuandaa programu za kitaifa za utayari wa ujifunzaji wa mtoto kabla ya kuingia Darasa la Kwanza ifikapo Juni 2028. | Idadi/Asilimia ya shule au Taasisi zinazotekeleza programu za kitaifa. | 69,017,250,000.00 | Julai 2027-Juni 2028 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |
| | | | Kuwajengea uwezo walimu kutambua na kusaidia watoto wenye changamoto za kisaikolojia na kijamii | Idadi/Asilimia ya walimu waliopewa mafunzo. | 91,822,950,000.00 | Julai 2027-Juni 2028 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | katika kipindi cha mpito ifikapo Juni 2028. | | | | za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |
| | | | Kuimarisha ujifunzaji wa Kihisia na Kijamii (SEL) katika Darasa la Kwanza na la Pili ifikapo Juni 2028. | Idadi/Asilimia ya shule au walimu wa Darasa la Kwanza na la Pili wanaoendesha shughuli za ujifunzaji zinazojumuisha Stadi za Kihisia na Kijamii (SEL). | 72,982,500,000.00 | Julai 2027- Juni 2028 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |
| | | | Kuelimisha wazazi kuhusu namna ya kuwaandaa watoto wao kuhimili mabadiliko ya mazingira ya shule ifikapo Juni 2030. | Asilimia ya wazazi/walezi walioelimishwa. | 0.00 | Julai 2027- Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Maendeleo ya Jamii. |
| | | **3.5: Ushirikiano wa Wazazi na Jamii katika Kipindi cha Mpito** | Kuandaa mikutano na warsha za wazazi kuhusu umuhimu wa kipindi cha mpito katika ujifunzaji wa Stadi za KKK ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya wazazi/walezi waliohudhuria mikutano na warsha. | 0.00 | Julai 2026- Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wanawake na Makundi Maalumu. |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kuhamasisha na kushirikisha jamii kuunga mkono mazingira rafiki ya kipindi cha mpito kwa watoto ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya jamii, wazazi, walezi na wadau waliohusika katika kuunda na kudumisha mazingira rafiki, salama na jumuishi. | 32,000,000.00 | Julai 2026-Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wanawake na Makundi Maalumu. |
| | | | Kutumia viongozi wa jamii na dini kama mabalozi wa kusaidia watoto kupenda shule ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya shule au jamii zinazoshirikisha viongozi wa jamii na dini. | 28,575,000.00 | Julai 2026-Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wanawake na Makundi Maalumu. |
| | | | Kufuatilia mchango wa wazazi na jamii katika kufanikisha kipindi cha mpito ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya shule au watoto ambapo mchango wa wazazi, walezi na jamii umefuatiliwa. | 74,000,000.00 | Julai 2026 - Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya maendeleo ya jamii, Jinsia Wanawake na Makundi Maalumu. |
| **Mahitaji ya Fedha kufikia Lengo** | | | | | **280 565 775 000.00** | | |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 4. | **Kuimarisha Tathmini ya Ujifunzaji wa KKK na Matumizi ya Ushahidi wa Kitaalam katika Uboreshaji wa Ufundishaji** | **4.1: Tathmini Endelevu ya Ujifunzaji katika Ngazi ya Darasa** | Kuandaa na kusambaza miongozo ya kitaifa ya tathmini endelevu ya Stadi za KKK kwa Darasa la Awali na Darasa la I-II ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya shule na walimu wanaopokea, kutumia na kutekeleza miongozo ya kitaifa. | 47,000,000.00 | Julai 2027 - Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |
| | | | Kuwajengea uwezo walimu kuandaa na kutumia tathmini shirikishi na zinazoelekezwa katika kumsaidia mwanafunzi kujifunza (*assessment for learning*) ifikapo Juni 2028. | Idadi/Asilimia ya walimu wa Darasa la Awali hadi Darasa la II waliopatiwa mafunzo | 91,822,950,000.00 | Julai 2027 - Juni 2028 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |
| | | | Kuimarisha matumizi ya tathmini za mara kwa mara darasani ili kubaini mapema changamoto za ujifunzaji wa Stadi za KKK ifikapo Juni 2028. | Idadi/Asilimia ya walimu wa Darasa la Awali hadi Darasa la II wanaotumia tathmini za mara kwa mara. | 0.00 | Julai 2027- Juni 2028 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kuwajengea walimu uwezo wa kutumia TEHAMA kurekodi, kuchambua na kutumia matokeo ya tathmini katika kupanga ufundishaji ifikapo Juni 2028. | Idadi/Asilimia ya walimu wa Darasa la Awali hadi Darasa la II waliopatiwa mafunzo. | 0.00 | Julai 2027-Juni 2028 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |
| | | | Kuweka utaratibu wa kutoa mrejesho wa maendeleo ya ujifunzaji kwa wanafunzi na wazazi ifikapo Juni 2028. | Idadi/Asilimia ya shule na walimu wa Darasa la Awali hadi Darasa la II waliotoa mrejesho kwa wanafunzi na wazazi. | 0.00 | Julai 2027-Juni 2028 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |
| | | **4.2: Tathmini za Kitaifa na za Shule kwa Ufuatiliaji wa Umahiri wa Stadi za KKK** | Kuboresha zana za tathmini za kitaifa na za shule ili kupima umahiri halisi wa Stadi za KKK badala ya kukariri ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya shule na walimu wanaotumia zana za tathmini zilizoboreshwa. | 44,550,000.00 | Julai 2029-Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kuoanisha tathmini za Stadi za KKK na viwango vya matarajio ya ujifunzaji kwa Elimu ya Awali hadi Darasa la Pili ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya shule na walimu wanaotumia tathmini za Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK). | 0.00 | Julai 2029-Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |
| | | | Kuendesha tathmini za sampuli (*sample-based assessments*) za Stadi za KKK kwa ajili ya ufuatiliaji wa kitaifa ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya shule na watoto walioshiriki katika tathmini. | 0.00 | Julai 2029-Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |
| | | | Kuchambua na kusambaza matokeo ya tathmini kwa ngazi za shule, kata, Halmashauri, mkoa na Taifa ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya matokeo ya tathmini za Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) yaliyochambuliwa na kusambazwa. | 100,200,000.00 | Julai 2029-Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kutumia matokeo ya tathmini kama msingi wa kupanga afua za Kitaifa na za maeneo maalum ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya sera, mipango au afua za kitaifa na za kieneo zinazopangwa kwa kuzingatia matokeo ya tathmini za Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK). | 0.00 | Julai 2029-Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |
| | | **4.3: Afua za Kurekebisha Ujifunzaji kwa Watoto Wenye Changamoto (TaRL/Catch-Up)** | Kuandaa mfumo wa kitaifa wa utekelezaji wa mbinu ya *Teaching at the Right Level* (TaRL) ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya shule na walimu waliojiunga na kutumia mfumo wa kitaifa wa TaRL. | 24,825,000.00 | Julai 2026-Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |
| | | | Kuwajengea uwezo walimu kutambua wanafunzi kulingana na kiwango chao halisi cha ujifunzaji wa Stadi za KKK ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya walimu wa Darasa la Awali hadi Darasa la II waliopata mafunzo. | 91,822,950,000.00 | Julai 2026-Juni 2027 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kuandaa makundi ya ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya wanafunzi badala ya darasa walilopo ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya walimu wa Darasa la Awali hadi Darasa la II wanaounda na kuendesha makundi ya ujifunzaji. | 0.00 | Julai 2026-Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |
| | | | Kutekeleza vipindi maalum vya kurekebisha ujifunzaji (*remedial and catch-up sessions*) ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya shule na walimu wa Darasa la Awali hadi Darasa la II wanaoendesha vipindi. | 0.00 | Julai 2026-Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |
| | | | Kufuatilia maendeleo ya wanafunzi waliopatiwa afua za TaRL na kurekebisha mbinu kulingana na matokeo ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya walimu wa Darasa la Awali hadi Darasa la II wanaofuatilia Maendeleo. | 74,000,000.00 | Julai 2026-Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |
| | | **4.4: Motisha na Uwajibikaji katika Matumizi ya Tathmini** | Kuweka mifumo ya kutambua na kuthamini walimu wanaotumia tathmini kuboresha ujifunzaji | Idadi/Asilimia ya walimu wa Darasa la Awali hadi Darasa la II waliotambuliwa na | 0.00 | Julai 2029-Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | wa Stadi za KKK ifikapo Juni 2030. | kuthaminiwa. | | | za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |
| | | | Kuhamasisha shule kutumia matokeo ya tathmini kama nyenzo ya kujifunza na si ya kuadhibu ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya shule na walimu wa Darasa la Awali hadi Darasa la II wanaotumia matokeo ya tathmini za Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK). | 0.00 | Julai 2026-Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |
| | | | Kuimarisha uwajibikaji wa Wadau wa Elimu katika kuboresha matokeo ya Stadi za KKK kwa kutumia ushahidi ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya Wadau wa Elimu (walimu, wasimamizi, wazazi, Halmashauri, mikoa na Wizara) wanaotumia data na ushahidi wa matokeo ya Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK). | 0.00 | Julai 2026-Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |
| | | | Kuweka utaratibu wa kujifunza kutokana na shule zinazofanya vizuri katika matumizi ya tathmini ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya shule na walimu wanaoshiriki katika utaratibu wa kujifunza kutokana na shule zinazofanya vizuri | 0.00 | Julai 2026-Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | (*School-to-School Learning*). | | | dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |
| | | | Kuandaa taarifa za robo mwaka za maendeleo ya ujifunzaji wa Stadi za KKK kwa umma na wadau ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya shule, Halmashauri, Mikoa na Wizara zinazotoa taarifa za robo mwaka. | 0.00 | Julai 2029-Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |
| | | **4.5: Ushirikishwaji wa Wazazi na Jamii katika Tathmini ya Ujifunzaji** | Kutoa elimu kwa wazazi kuhusu namna ya kuelewa matokeo ya tathmini ya Stadi za KKK ya watoto wao ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya Wazazi na Walezi waliopatiwa mafunzo au Elimu. | 0.00 | Julai 2029-Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |
| | | | Kuandaa mifumo rahisi ya kuwapa wazazi mrejesho wa maendeleo ya watoto wao ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya shule zinazotumia mifumo rahisi na ya mara kwa mara ya kutoa mrejesho. | 0.00 | Julai 2029-Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kuwashirikisha wazazi katika kupanga afua za kuwasaidia watoto wenye changamoto za ujifunzaji ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya wazazi/walezi waliohusika katika kupanga na kutekeleza afua husika. | 0.00 | Julai 2029-Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |
| | | | Kuhamasisha jamii kuunga mkono jitihada za kuboresha ujifunzaji wa Stadi za KKK kwa kuzingatia ushahidi uliopo ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya jamii, viongozi wa kijamii na dini, na wadau wengine wanaoshirikiana na shule. | 0.00 | Julai 2029-Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |
| | | | Kujenga uelewa wa pamoja kuwa tathmini ni nyenzo ya kuboresha ujifunzaji na ufundishaji ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya walimu, wasimamizi, wazazi, na jamii waliopatiwa mafunzo au elimu. | 0.00 | Julai 2029-Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Taasisi za Elimu. |
| **Mahitaji ya Fedha kufikia Lengo** | | | | | **183,936,475,000.00** | | |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 5 | **Kuimarisha Matumizi ya TEHAMA, Takwimu na Ubunifu katika Utekelezaji wa Stadi za KKK** | **5.1: Kuimarisha Mifumo ya Takwimu za Ujifunzaji wa Stadi za KKK** | Kuboresha mifumo ya TEHAMA kama vile BEMIS na SIS ili kuanzisha Dashibodi ya Taifa ya KKK na kujumuisha viashiria vya Stadi za KKK ifikapo Juni 2029. | Idadi/Asilimia ya shule na Halmashauri zinazotumia mifumo ya TEHAMA (kama BEMIS na SIS). | 14,625,000.00 | Julai 2028-Juni 2029 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Sekta Binafsi. |
| | | | Kuoanisha mifumo ya takwimu ya ujifunzaji wa Stadi za KKK na mifumo mingine ya kitaifa ya elimu na maendeleo ya mtoto ifikapo Juni 2029. | Idadi/Asilimia ya mifumo ya takwimu ya ujifunzaji wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) katika shule za awali na msingi iliyooanishwa. | 0.00 | Julai 2028-Juni 2029 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Sekta Binafsi. |
| | | | Kutoa mafunzo ya uandaaji, ukusanyaji na uthibitishaji wa takwimu za ujifunzaji na tathmini za Stadi za KKK katika ngazi ya shule ifikapo Juni 2029. | Idadi/Asilimia ya shule zilizopatiwa na kutumia miongozo rasmi. | 91,822,950,000.00 | Julai 2028-Juni 2029 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Sekta Binafsi. |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kukusanya takwimu za Stadi za KKK kwa wakati na ulinganifu wa kitaifa ifikapo Juni 2029. | Idadi/Asilimia ya Walimu, Walimu Wakuu na Maafisa Elimu waliopata mafunzo. | 80,420,100,000.00 | Julai 2028-Juni 2029 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Sekta Binafsi. |
| | | **5.2: Matumizi ya Takwimu katika kufanya Maamuzi ya Kisera na Kitaaluma** | Kuwajengea uwezo watunga Sera na Wasimamizi wa Elimu kutumia takwimu za Stadi za KKK katika kupanga afua stahiki | Ripoti za mipango na Sera zilizoandaliwa kwa kutumia takwimu za KKK | 390,150,000.00 | Julai 2028-Juni 2029 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Sekta Binafsi. |
| | | | Kuandaa taarifa za robo mwaka ngazi za Halmashauri na taarifa ya mwaka ya Kitaifa kuhusu hali ya ujifunzaji wa Stadi za KKK. | Idadi/Asilimia ya taarifa zinazotayarishwa na kusambazwa za kwa muda muafaka. | 0.00 | Julai 2026-Juni 2029 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Sekta Binafsi. |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kutumia matokeo ya takwimu kubaini maeneo yenye changamoto kubwa ya ujifunzaji duni (*learning poverty*). Ifikapo Juni 2029. | Idadi na uwiano wa maeneo (Mikoa/ Halmashauri/Shule) yaliyobainishwa na kupewa kipaumbele kwa afua za kielimu. | 0.00 | Julai 2026-Juni 2029 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Sekta Binafsi. |
| | | | Kuhamasisha utamaduni wa kufanya maamuzi yanayotegemea ushahidi katika ngazi zote za utekelezaji wa mkakati ifikapo Juni 2029. | Idadi ya mihtasari inyoonesha taarifa ya maamuzi, mipango na afua za utekelezaji wa mkakati katika ngazi zote (Taifa, Mkoa, Halmashauri, Shule). | 0.00 | Julai 2026-Juni 2029 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Sekta Binafsi. |
| | | **5.3: Matumizi ya TEHAMA katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi za KKK** | Kuwezesha shule kutumia TEHAMA kusaidia ujifunzaji na ufundishaji wa Stadi za KKK kwa watoto walioko nyuma kielimu ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya shule zinazotumia TEHAMA. | 292,500,000.00 | Julai 2026-Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Sekta Binafsi. |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kufuatilia mchango wa TEHAMA katika kuboresha umahiri wa Stadi za KKK kwa wanafunzi ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya shule au wanafunzi waliothibitishwa kutumia TEHAMA na kuthibitishwa kuboresha umahiri wa Stadi za KKK. | 74,000,000.00 | Julai 2026-Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Sekta Binafsi. |
| | | **5.4: Ubunifu wa Kielimu na Utatuzi Endelevu wa Stadi za KKK** | Kuweka majukwaa ya kubadilishana ubunifu wa walimu katika ngazi ya shule, Kata, Halmashauri, Mkoa na Taifa ifikapo Juni 2030. | Idadi ya majukwaa yaliyoanzishwa | 752,000,000.00 | Julai 2029-Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Sekta Binafsi. |
| | | | Kushirikisha Taasisi za utafiti, vyuo na Sekta Binafsi katika kuendeleza mbinu bunifu za Stadi za KKK ifikapo Juni 2030. | Kuwepo kwa mpango wa Stadi za KKK unaoshirikisha Taasisi za utafiti, Vyuo na Sekta Binafsi, na asilimia za shule zinazotekeleza mpango huu. | 0.00 | Julai 2029-Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Sekta Binafsi. |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kujaribu (Piloting) na kupanua mbinu bunifu zilizothibitishwa kuboresha ujifunzaji wa Stadi za KKK ifikapo Juni 2030. | Kuwepo kwa mbinu bunifu za ufundishaji wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) zilizothibitishwa kupitia majaribio | 535,000,000.00 | Julai 2029-Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Sekta Binafsi. |
| | | | Kutambua na kuthamini ubunifu bora wa walimu na shule katika utekelezaji wa Stadi za KKK ifikapo Juni 2030. | Asilimia au idadi ya walimu na shule zilizotambuliwa | 0.00 | Julai 2029-Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Sekta Binafsi. |
| **Mahitaji ya Fedha kufikia Lengo** | | | | | **174,301,325,000.00** | | |
| 6. | **Kuimarisha Ustawi wa Mtoto, Chakula na Lishe na Ushirikiano wa Jamii katika Ujifunzaji wa Stadi za KKK** | **6.1: Kuimarisha Huduma za Chakula na Lishe Shuleni** | Kuimarisha utekelezaji wa mpango wa kitaifa wa chakula na lishe shuleni kwa madarasa ya Elimu ya Awali hadi Darasa la Pili ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya shule za Elimu ya Awali hadi Darasa la Pili zinazotekeleza mpango. | 0.00 | Julai 2026 - Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Afya, Kilimo na Taasisi za Elimu. |
| | | | Kutenga na kusimamia ruzuku ya chakula shuleni ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya shule zinazopokea na kusimamia ruzuku ya chakula. | 0.00 | Julai 2026 - Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Wizara ya Afya, Taasisi za |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | Elimu, Wizara ya Kilimo. |
| | | | Kushirikisha Wazazi, Walezi na Jamii katika kuchangia chakula kwa utaratibu unaozingatia mazingira ya kijamii na kiuchumi ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya shule zinazoshirikisha Wazazi, Walezi na Jamii. | 0.00 | Julai 2026 - Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Wizara ya Afya, Taasisi za Elimu, Wizara ya Kilimo. |
| | | | Kukuza miradi ya uzalishaji wa chakula shuleni kama vile bustani za mbogamboga, miti ya matunda pamoja na mashamba ya kilimo cha mazao ya chakula ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya shule zinazotekeleza miradi ya uzalishaji wa chakula. | 0.00 | Julai 2026 - Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Wizara ya Afya, Taasisi za Elimu, Wizara ya Kilimo. |
| | | | Kushirikisha wadau wa maendeleo na sekta Binafsi katika kusaidia upatikanaji wa chakula na lishe shuleni ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya shule zinazopatiwa msaada wa chakula na lishe kutoka kwa wadau wa maendeleo na Sekta Binafsi. | 0.00 | Julai 2026 - Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Wizara ya Afya, Taasisi za Elimu, Wizara ya Kilimo. |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **6.2: Kuimarisha Afya, ulinzi Usalama na Ustawi wa Mtoto Shuleni** | Kuhakikisha utekelezaji wa miongozo ya Dawati la ulinzi na usalama wa mtoto, Afya, usafi na mazingira katika shule za Elimu ya Awali na Msingi ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya shule za Elimu ya Awali na msingi zinazotekeleza kikamilifu miongozo. | 0.00 | Julai 2026 - Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wizara ya Afya na Wizara ya Mambo ya Ndani. |
| | | | Kuimarisha huduma za Afya ya msingi shuleni kwa kushirikiana na Sekta ya Afya ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya shule zinazotoa huduma za Afya ya msingi. | 0.00 | Julai 2026- Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wizara ya Afya |
| | | | Kuanzisha na kuimarisha mifumo ya ulinzi wa mtoto dhidi ya ukatili, unyanyasaji na unyonyaji ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya shule au Taasisi za Elimu zinazotekeleza kikamilifu mifumo ya ulinzi wa mtoto. | 0.00 | Julai 2026- Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wizara ya Afya. |
| | | | Kuwajengea uwezo walimu kutambua na kushughulikia changamoto za ustawi wa watoto ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya walimu waliopewa mafunzo. | 91,822,950,000.00 | Julai 2026- Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wizara ya Afya |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kuelimisha watoto kuhusu usalama wao, Afya na ustawi kwa kuzingatia umri wao ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya watoto walioelimishwa. | 0.00 | Julai 2026- Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wizara ya Afya. |
| | | **6.3: Kuimarisha Ushirikiano wa Wazazi na Walimu (UWaWa)** | Kuimarisha utekelezaji wa mwongozo wa Ushirikiano wa Walimu na Wazazi (UWaWa) katika shule zote za Awali na Msingi. | Idadi/Asilimia ya shule za Elimu ya Awali na msingi zinazotekeleza kikamilifu mwongozo. | 0.00 | Julai 2026- Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. |
| | | | Kuandaa mikutano ya nusu mwaka kati ya walimu na wazazi kujadili maendeleo ya ujifunzaji wa Stadi za KKK ifikapo Juni 2030. | Idadi/asilimia ya mikutano ya walimu na wazazi inayofanyika. | 0.00 | Julai 2026- Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi maalum. |
| | | | Kutoa Elimu kwa wazazi na walezi juu ya umuhimu wa chakula na lishe bora kwa watoto na elimu kwa jamii, wazazi/walezi juu ya Maendeleo ya watoto katika kujifunza Stadi | Idadi/Asilimia ya wazazi, walezi na wanajamii walioelimishwa au kushiriki. | 0.00 | Julai 2026- Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Wizara ya Afya, Taasisi za Elimu, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | za KKK Ili wafanye ufuatiliaji ifikapo Juni 2030. | | | | Makundi Maalum Wizara ya Afya, na Wizara ya Kilimo. |
| | | | Kuanzisha mifumo rahisi ya mawasiliano kati ya shule na wazazi kuhusu maendeleo ya watoto ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya shule zilizounda na kuanzisha mifumo rahisi ya mawasiliano. | 0.00 | Julai 2026 - Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Wizara ya Afya, Taasisi za Elimu, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi maalum Wizara ya Afya, na Wizara ya Kilimo. |
| | | | Kuhamasisha uwajibikaji wa pamoja wa walimu na wazazi katika mafanikio ya Stadi za KKK ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya walimu na wazazi wanaoshiriki kikamilifu katika mipango, shughuli na ufuatiliaji. | 0.00 | Julai 2026 - Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Wizara ya Afya, Taasisi za Elimu, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi maalum Wizara ya Afya, na Wizara ya Kilimo. |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **6.4: Ujumuishaji na Ulinzi wa Makundi Maalum ya Watoto** | Kubaini na kufuatilia watoto wenye ulemavu, walio katika mazingira hatarishi na wenye ulemavu na walio katika mazingira magumu ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya watoto wenye ulemavu, walio katika mazingira hatarishi na mazingira magumu. | 75,000 000.00 | Julai 2026 - Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Wizara yenye dhamana ya Maendeleo ya Jamii, Wizara ya Afya, na Wizara ya Mambo ya ndani. |
| | | | Kuhakikisha mazingira ya shule yanazingatia mahitaji ya watoto wote bila ubaguzi ifikapo Juni 2030 | Idadi/Asilimia ya shule zinazounda na kudumisha mazingira ya kujifunzia. | 0.00 | Julai 2026 - Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wizara ya Afya |
| | | | Kuimarisha huduma za ushauri nasaha na msaada wa kijamii kwa watoto wenye changamoto ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya shule au vituo vya elimu zinavyotoa huduma za ushauri, nasaha na msaada wa Jamii. | 0.00 | Julai 2026 - Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wizara ya Afya. |
| | | | Kushirikiana na Sekta ya Ustawi wa Jamii kutoa afua jumuishi kwa watoto wenye mahitaji maalum ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya shule au Taasisi za Elimu zinazoshirikiana na Sekta ya Ustawi wa Jamii. | 0.00 | Julai 2026 - Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wizara ya Afya. |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Miongozo ya ulinzi wa mtoto shuleni ifikapo Juni 2030. | Idadi/Asilimia ya shule zinazofuatiliwa na kutathminiwa. | 74,000,000.00 | Julai 2026 - Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wizara ya Afya. |
| **Mahitaji ya Fedha kufikia Lengo** | | | | | **91,971,950,000.00** | | |
| 7. | **Kuimarisha Uongozi, Uratibu, Rasilimali na Uendelevu wa Mkakati wa KKK** | **7.1: Uongozi na Uratibu wa Kitaifa wa Mkakati wa Stadi za KKK** | Kuanzisha na kuimarisha mfumo wa uongozi wa kitaifa wa mkakati wa Stadi za KKK chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ifikapo Juni 2027. | Kuwepo na utekelezaji wa mfumo wa uongozi wa kitaifa. | 25,000,000.00 | Julai 2026-Juni 2027 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Wizara yenye dhamana ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Sekta Binafsi, Taasisi za Elimu, Wadau wa Maendeleo, na Wizara yenye dhamana na Fedha |
| | | | Kuunda Kamati ya Kitaifa ya Uratibu wa Stadi za KKK itakayojumuisha Sekta husika, Taasisi za Umma na Wadau wa Maendeleo ifikapo Juni 2027. | Kuwepo kwa Kamati ya Kitaifa ya Uratibu wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK). | 30,000,000.00 | Julai 2026-Juni 2027 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Sekta Binafsi. |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kuweka bayana majukumu na uwajibikaji wa wazi kwa kila ngazi ya utekelezaji (Taifa, Mkoa, Halmashauri Kata na Shule) ifikapo Juni 2027. | Uwepo na mfumo wa utekelezaji wa majukumu kwa ngazi ya Taifa hadi ngazi ya Shule. | 0.00 | Julai 2026-Juni 2027 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Taasisi za Elimu. |
| | | | Kuandaa miongozo ya utekelezaji wa mkakati wa Stadi za KKK kwa ngazi zote ifikapo Juni 2027. | Idadi ya Miongozo ya utekelezaji wa mkakati wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK). | 80,000,000.00 | Julai 2026-Juni 2027 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, na Wizara yenye dhamana na Maendeleo ya Jamii. |
| | | | Kuimarisha uratibu kati ya Wizara ya Elimu TAMISEMI na Sekta nyingine zinazohusika na maendeleo ya mtoto ifikapo Juni 2030. | Kuwepo na utekelezaji wa mifumo ya uratibu iliyoimarishwa kati ya Wizara ya Elimu, TAMISEMI na sekta nyingine. | 0.00 | Julai 2026-Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Wizara ya Mipango na Fedha, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Sekta Binafsi, Taasisi za Elimu, Wadau wa Maendeleo. |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **7.2: Uratibu wa Kisekta Mtambuka na Ushirikiano wa Wadau** | Kuimarisha uratibu wa utekelezaji wa Stadi za KKK kati ya Sekta za Elimu na Wizara/Taasisi zinazohusika na utekelezaji wa Stadi za KKK ifikapo Juni 2030. | Kuwepo na utekelezaji wa mifumo ya uratibu (Kamati au Mifumo ya pamoja ya Mipango, Ufuatiliaji na Taarifa) . | 99,750,000.00 | Julai 2029-Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM -TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Wizara yenye dhamana na Fedha, Wizara yenye dhamana ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Sekta Binafsi, Wadau wa Maendeleo. |
| | | | Kufanya mapitio ya miongozo mbalimbali ya ufundishaji na ujifunzaji wa mtoto ili kupata mwongozo mmoja unaojitosheleza ifikapo Juni 2028. | Kuwepo kwa mwongozo mmoja uliofanyiwa mapitio. | 80,000,000.00 | Julai 2027-Juni 2028 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Sekta Binafsi, Taasisi za Elimu, Wadau wa Maendeleo. |
| | | | Kuimarisha ushirikishwaji wa wadau wa maendeleo katika utekelezaji wa afua za Stadi za KKK ifikapo Juni 2030. | Asilimia ya wadau wa maendeleo walioshirikishwa. | 0.00 | Julai 2026-Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | Teknolojia, Sekta Binafsi, Taasisi za Elimu, Wadau wa Maendeleo. |
| | | | Kuanzisha majukwaa ya wadau kwa ajili ya kubadilishana taarifa, uzoefu na mbinu bora za ufundishaji na ujifunzaji wa Stadi za KKK ifikapo Juni 2026. | Idadi/Asilimia ya majukwaa ya wadau yaliyoanzishwa. | 0.00 | Novemba 2025 – Juni 2026 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Sekta Binafsi, Taasisi za Elimu, Wadau wa Maendeleo. |
| | | **7.3: Ugharamiaji na Uendelevu wa Kifedha wa Mkakati wa Stadi za KKK** | Kutenga bajeti maalum ya kitaifa ya utekelezaji wa mkakati wa Stadi za KKK ifikapo Aprili 2030. | Kuwepo kwa bajeti maalum. | 331,127,745,000.00 | Januari 2026 - Aprili 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi za Elimu, Sekta Binafsi. |

| Na. | Lengo | Mkakati | Shabaha | Viashiria | Rasilimali | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kuweka miongozo ya kugharamia shughuli za Stadi za KKK katika ngazi ya Halmashauri na Shule ifikapo Juni 2028. | Idadi ya miongozo ya kugharamia shughuli za KKK iliyowekwa. | 80,000,000.00 | Juni 2026 - Juni 2028 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Wizara yenye dhamana na Fedha, Sekta Binafsi. |
| | | | Kuhamasisha uwekezaji wa wadau wa maendeleo na Sekta Binafsi katika afua za Stadi za KKK ifikapo Juni 2030. | Kiasi/Asilimia ya rasilimali za kifedha au msaada wa kiufundi uliopatikana kutoka kwa wadau wa maendeleo na Sekta Binafsi. | 0.00 | Julai 2027 - Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi za Elimu, Sekta Binafsi. |
| | | | Kuendeleza mifumo ya ubunifu ya ugharamiaji (blended financing) kwa Elimu ya Awali na Msingi ifikapo Juni 2030. | Kuwepo na matumizi ya mifumo ya ubunifu ya ugharamiaji (blended financing) iliyoundwa. | 76,500,000.00 | Julai 2029 - Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWM-TAMISEMI, Sekta Binafsi. |
| | | | Kufuatilia matumizi ya rasilimali fedha ili kuhakikisha thamani halisi ya fedha (*Value for Money*) ifikapo Juni 2030 | Asilimia ya miradi au shughuli za elimu kuhusu Stadi za KKK zilizofuatiliwa na kutathminiwa | 74,000,000.00 | Julai 2026- Juni 2030 | Wizara yenye dhamana ya Elimu, Wizara yenye dhamana ya OWN-TAMISEMI, Wizara yenye dhamana ya Fedha na Mipango |
| **Mahitaji ya Fedha kufikia Lengo** | | | | | **331,672,995,000.00** | | |
| **Jumla Kuu ya Fedha ya Utekelezaji** | | | | | **1,927,082,470,000.00** | | |

## 4.0 UFUATILIAJI NA TATHMINI

Utekelezaji wa mpango mkakati wa kisayansi wa kuhakikisha kila mtoto afikapo Darasa la Tatu ana uwezo wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK); unahitaji ufuatiliaji na tathmini ili kutoa taarifa ya kufikiwa kwa malengo yake. Lengo kuu la Ufuatiliaji na Tathmini ni kutoa mwongozo wa utekelezaji wa Mpango Mkakati ili kuleta utekelezaji wenye tija na ufanisi.

Ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mpango mkakati huu ni nyenzo muhimu katika kuweka utaratibu au mfumo (framework) wa kujenga msingi wa kutambua ufanisi katika utekelezaji wake. Aidha, unalenga pia kupata taarifa za utendaji na ufanisi, ambazo zitatumika kufanya uamuzi muhimu na kwa wakati kuhusu maendeleo ya ujifunzaji wa Stadi za KKK nchini. Ufuatiliaji na tathmini hii ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wa kujenga uwezo wa ujifunzaji wa Stadi za KKK. Aidha, ufuatiliaji na tathmini utazingatia mchakato wa utekelezaji, matokeo ya awali ya utekelezaji, na manufaa yatokanayo na matokeo ya malengo yaliyokusudiwa ndani ya mpango mkakati kwa kutumia viashiria vilivyobainishwa ili kuwa na ufanisi uliokusudiwa.

Mpango mkakati umeainisha nafasi, majukumu na wajibu wa kila mdau kuanzia ngazi ya Serikali Kuu hadi Mamlaka za Serikali za Mitaa, Shule, Sekta Binafsi na Washirika wa Maendeleo ya kielimu. Ufuatiliaji na Tathmini utaratibiwa na Wizara yenye dhamana ya elimu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo Wizara nyingine, mashirika na Taasisi za Serikali na zisizo za Serikali, washirika wa maendeleo wa ndani na nje, jamii na wadau wengine wa elimu na mafunzo.

### 4.1 Malengo Mahsusi ya Ufuatiliaji na Tathmini

Malengo mahususi ni kama yafuatayo:

(i) Kuweka shabaha na viashiria vya upimaji wa maendeleo ya utekelezaji wa Mpango Mkakati;

(ii) Kutoa mwongozo wa ushiriki wa wadau katika utekelezaji, ufuatiliaji na tathmiini ya mpango Mkakati wa utekelezaji wa Mpango Mkakati wa kisayansi wa

kuhakikisha kila mtoto afikapo Darasa la Tatu aweze Kusoma, Kuandika na Kuhesabu;

(iii) Kuthibiti matumizi ya rasilimali wakati wa utekelezaji; na

(iv) Kuchukua hatua za haraka katika eneo linalobainika kuwa na changamoto ya utekelezaji.

## 4.2 Maeneo na Vipengele Muhimu vya Ufuatiliaji na Tathmini

(a) Utekelezaji wa mkakati utafanikisha malengo yake na kuleta manufaa yaliyokusudiwa. Hivyo, ni muhimu kuwa na mfumo wa ufuatiliaji na tathmini utakaotoa mwongozo wa utekelezaji wa mpango mkakati kuanzia hatua ya awali kwa ufanisi.

Malengo mahsusi kama yalivyobainishwa yatafuatiliwa na kutathminiwa kwa kuzingatia:

(i) Viashiria vya utendaji *(performance indicators*) katika ngazi mbalimbali za matokeo (*outcome, output, process, input*);

(ii) Taarifa za utendaji (*performance reports*) ambazo zitatolewa kwa nyakati tofauti (robo mwaka, nusu mwaka, mwaka, muda wa kati wa mkakati na tamati);

(iii) Mapitio ya utendaji (*performance review*) kwa njia ya mikutano ya mapitio (*review meetings*) na tathmini za robo mwaka (*rapid appraisals*); na

(iv) Tathmini ya utendaji (*performance evaluation*) kwa njia ya upembuzi yakinifu (*feasibility study*), tathmini endelevu (*process evaluation*), tathmini mahsusi (*thematic evaluation*), ukaguzi wa utendaji (*performance audit*), tathmini ya matokeo ya mpango mkakati (*outcome evaluation*) na tathmini ya manufaa ya

utekelezaji wa mpango mkakati (*impact evaluation*).

(b) Ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mpango mkakati unatambua nafasi, majukumu na wajibu wa kila mdau kama ilivyoainishwa.

(c) Ufuatiliaji na tathmini utazingatia miundo na mifumo ya kiTaasisi ya ufuatiliaji na tathmini kwa ngazi ya Taifa, Mkoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Shule kutegemea Mpango Mkakati wa kila Taasisi.

(d) Ufuatiliaji na tathmini utazingatia mpango na ratiba ya Serikali ya utoaji wa taarifa na mpango na ratiba ya utekelezaji ya Taasisi husika. Ratiba na mipango hiyo itahusisha: ratiba ya utoaji taarifa za ndani na nje ya Taasisi; mpango wa ufuatiliaji; tathmini na mikutano ya mapitio ya utekelezaji wa majukumu.

(e) Taarifa na takwimu muhimu za utekelezaji wa mpango mkakati zitakusanywa na kila mdau kwa ngazi mbalimbali za utekelezaji. Taarifa hizo zitakusanywa kwa kutumia mfumo uliopo wa ukusanyaji taarifa kuanzia ngazi ya shule hadi Taifa. Wadau watawajibika kutoa ushirikiano wakati wa ukusanyaji wa taarifa na takwimu. Lengo ni kuhakikisha kila mdau anashiriki kikamilifu kwa kutoa takwimu zitakazotumika kupima utendaji kwa kuzingatia viashiria vya utendaji.

(f) Taarifa na takwimu zitakazokusanywa kutoka katika ngazi mbalimbali za utekelezaji wa mpango mkakati zitachambuliwa ili kupata taarifa ya utekelezaji kwa kipindi husika. Taarifa hizo zitakuwa msingi wa kufanya uamuzi kuhusu utekelezaji wa mpango mkakati.

(g) Taarifa za ufuatiliaji na tathmini zitaandaliwa kwa kila robo mwaka na taarifa ya jumla itatolewa kwa mwaka. Mfumo wa utoaji taarifa utaanza katika ngazi ya shule hadi Taifa.

(h) Taarifa za ufuatiliaji na tathmini zitashirikisha wadau kwa ajili ya mrejesho wa hali ya utekelezaji wa mpango mkakati na matokeo yake kwa ngazi mbalimbali kisha kupata maoni ya kuendelea kuimarisha utekelezaji wa mpango mkakati na kuona endapo ni sawa wadau watahusika katika kuandaa taarifa.

## 5.0 MPANGO ENDELEVU WA MKAKATI

Elimu ya msingi ni nguzo ya maendeleo ya Taifa, ikiwemo ustawi wa kijamii, kiuchumi, na kimaadili wa watoto. Mpango Mkakati huu umeundwa kwa lengo la kuhakikisha kila mtoto anapata ujuzi thabiti wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kufikia Darasa la Tatu. Utekelezaji wake unazingatia mbinu za kisayansi, tathmini endelevu na ufuatiliaji wa kina ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Mpango unalenga kutoa fursa sawa kwa watoto wote bila kujali asili yao ya kijamii, kijiografia au kiuchumi, kuhakikisha kila mtoto anafanikiwa kielimu. Hatua hizi zinajumuisha mafunzo ya walimu, vifaa vya kufundishia na usimamizi makini wa maendeleo ya ujifunzaji ili kuhakikisha mafanikio endelevu ya kila mtoto. Jedwali lifuatalo linafafanua mikakati endelevu ya kutekeleza Mkakati wa Kisayansi wa Kuhakikisha kila Mtoto afikapo Darasa la III anaweza Kusoma, Kuandika na Kuhesabu:

| Na. | Mpango Mkakati | Mkakati Endelevu | Nyenzo | Matokeo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | **Elimu ya Awali Jumuishi na Ujifunzaji Unaomlenga Mtoto**. | • Kuendeleza matumizi ya mbinu shirikishi zinazozingatia mahitaji ya kila mtoto kama michezo ya kielimu, hadithi, nyimbo, vitendo na majaribio rahisi.<br>• Kuendeleza ufundishaji unaozingatia kasi, uwezo na mtindo wa ujifunzaji wa kila mtoto.<br>• Kuweka mazingira ya darasa | • Nyenzo za Ufundishaji na Ujifunzaji.<br>• Nyenzo za michezo na sanaa.<br>• Nyenzo za TEHAMA.<br>• Nyenzo za Elimu Jumuishi.<br>• Nyenzo za mazingira ya kujifunzia.<br>• Nyenzo za | Kuwepo kwa misingi imara ya Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa watoto wote bila ubaguzi. |

| Na. | Mpango Mkakati | Mkakati Endelevu | Nyenzo | Matokeo |
|---|---|---|---|---|
| | | yanayochochea udadisi, ubunifu na ushiriki wa kila mtoto.<br><br>• Kuhakikisha watoto wote wakiwemo wenye mahitaji maalum wanapata fursa sawa ya kushiriki katika ujifunzaji.<br><br>• Kubuni na kutumia nyenzo rahisi na zinazobadilika kulingana na mahitaji ya watoto mbalimbali.<br><br>• Kuimarisha uelewa wa walimu kuhusu elimu jumuishi na utofauti wa watoto.<br><br>• Kutoa mafunzo endelevu ya vitendo kuhusu ujifunzaji unaomlenga mtoto na elimu jumuishi.<br><br>• Kutumia mbinu ya mafunzo kazini (coaching na mentoring) katika vituo vya elimu ya awali.<br><br>• Kuendeleza Jumuiya za Ujifunzaji (JzK). | tathmini rafiki kwa mtoto.<br>• Nyenzo za mafunzo kwa walimu | |
| 2. | **Umahiri wa Walimu na Ubora wa Ufundishaji wa Stadi za KKK** | • Kuendesha mafunzo ya robo mwaka kuhusu ufundishaji wa KKK kwa kutumia mbinu za bunifu na Mtaala ulioboreshwa. | • Miongozo ya Ufundishaji.<br><br>• Moduli za mafunzo ya KKK.<br><br>• Vitabu vya mbinu za kisasa za | • Kuongezeka umahiri wa kitaaluma na kiufundishaji wa walimu wa KKK.<br><br>• Kuimarika kwa |

| Na. | Mpango Mkakati | Mkakati Endelevu | Nyenzo | Matokeo |
|---|---|---|---|---|
| | | • Kutumia mbinu ya mafunzo ya mnyororo (cascade model) yenye viwango vya ubora na ufuatiliaji.<br><br>• Kuhakikisha mafunzo yanazingatia vitendo (activity-based training) badala ya nadharia pekee.<br><br>• Kuimarisha mfumo wa walimu wakufunzi (coaches) na wasimamizi wa KKK katika ngazi ya shule na kata.<br>• Kufanya ufuatiliaji wa darasani unaolenga kusaidia walimu kuboresha ufundishaji.<br><br>• Kutoa mrejesho wa robo mwaka unaotokana na ushahidi wa matokeo ya ufundishaji na ujifunzaji. | ufundishaji.<br><br>• Zana za tathmini ya KKK.<br><br>• *Portfolio* za kazi za wanafunzi.<br><br>• *Dashboard* za kufuatilia maendeleo ya KKK | matumizi bora ya mbinu za kisayansi na data katika ufundishaji.<br><br>• Kuimarika kwa uwezo wa kujiamini katika kufundisha KKK.<br><br>• Kujengeka kwa utamaduni wa ujifunzaji endelevu kwa walimu wa KKK.<br><br>• Kuwepo kwa maandalio ya ufundishaji yaliyoboreshwa. |
| 3. | **Mwendelezo wa Ujifunzaji na kipindi cha mpito katika Darasa la Awali na Elimu ya Msingi** | • Kuoanisha malengo ya ujifunzaji wa Darasa la Awali na matarajio ya Darasa la Kwanza, hasa katika Stadi za Lugha na Kuhesabu.<br><br>• Kuhakikisha mbinu za ujifunzaji unaomlenga mtoto zinaendelea kutumika Darasa la I.<br><br>• Kuandaa miongozo ya pamoja ya | • Miongozo ya walimu kuhusu mbinu shirikishi na za michezo.<br><br>• Vitabu vya mwanafunzi vinavyozingatia umri na maendeleo ya mtoto.<br><br>• Zana za tathmini endelevu za maendeleo ya mtoto. | • Mpito laini kutoka Darasa la Awali kwenda Darasa la Kwanza.<br><br>• Kuongezeka kwa ujasiri na kujiamini kwa mtoto anapoanza elimu ya msingi.<br><br>• Kuimarika kwa |

| Na. | Mpango Mkakati | Mkakati Endelevu | Nyenzo | Matokeo |
|---|---|---|---|---|
| | | ufundishaji kwa walimu wa Darasa la Awali na Darasa la I.<br>• Kuanzisha na kuendeleza mfumo wa kukusanya na kuhamisha taarifa za maendeleo ya mtoto kutoka Darasa la Awali kwenda Darasa la I.<br>• Kutumia taarifa hizo kupanga ufundishaji unaozingatia mahitaji halisi ya wanafunzi.<br>• Kufuatilia maendeleo ya ujifunzaji wa KKK katika miezi ya mwanzo ya Darasa la I.<br>• Kutumia matokeo ya tathmini kubaini mapengo ya mpito na kuchukua hatua za maboresho.<br>• Kuendeleza maboresho ya mpango wa mpito kulingana na ushahidi wa utekelezaji. | • Madarasa yenye miundombinu rafiki kwa watoto.<br>• Huduma za ushauri nasaha kwa watoto.<br>• Ripoti za mpito wa mwanafunzi kutoka Darasa la Awali kwenda la Kwanza. | Stadi za KKK kulingana na umri.<br>• Maendeleo ya kijamii na kihisia.<br>• Kupungua kwa utoro na kuacha shule mapema katika madarasa ya mwanzo |
| 4. | **Tathmini ya Ujifunzaji na Afua Lengwa za Kuboresha Stadi za KKK** | • Kutumia mbinu sahihi za tathmini za Robo Mwaka.<br>• Kuwezesha mtoto kushiriki katika tathmini kupitia mbinu za kujitathmini na kujieleza kuhusu maendeleo ya ujifunzaji wake.<br>• Kuandaa mbinu za | • Fomu za tathmini ya awali ya KKK.<br>• Vifaa vya tathmini endelevu.<br>• Zana za kuchambua matokeo.<br>• Nyenzo za | • Kuimarika kwa Stadi za msingi za KKK.<br>• Kuongezeka kwa mahusiano chanya kwa jamii.<br>• Uboreshaji wa mbinu za kufundishia kulingana na |

| Na. | Mpango Mkakati | Mkakati Endelevu | Nyenzo | Matokeo |
|---|---|---|---|---|
| | | tathmini zinazojumuisha kazi za vitendo, michezo ya kielimu na maswali ya mafunzo.<br><br>• Kuweka mpango wa utekelezaji wa afua shuleni kulingana na matokeo ya tathmini.<br><br>• Kubaini mapengo ya ujifunzaji na kupanga ufundishaji wa marekebisho (remedial lessons).<br><br>• Kuendeleza mpangilio wa kufundisha Stadi za KKK kwa kutumia data ya mwanafunzi Binafsi. | ubunifu (Karatasi, rangi, plastiki) kusaidia uandishi na kuhesabu. | matokeo.<br><br>• Kuongezeka kwa mahudhurio na ushirikiano wa wanafunzi. |
| 5. | **Takwimu, TEHAMA na Uamuzi Unaotegemewa** | • Kuweka mfumo wa kudumu wa kukusanya taarifa za maendeleo ya kila mtoto (*Child Level Data*) mara kwa mara.<br><br>• Kuhakikisha kwamba takwimu na taarifa nyingine zinazokusanywa zinashirikisha pande zote husika na haziathiriwi na upendeleo wowote.<br><br>• Kufuatilia viashiria vya msingi vya KKK.<br><br>• Kutumia mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya kuingiza, kuchambua, na kufuatilia takwimu | • Daftari la maendeleo ya mwanafunzi<br><br>• Chati na Grafu<br><br>• Ripoti za takwimu kwa walimu, uongozi wa shule na maafisa elimu<br><br>• Program za TEHAMA za elimu (apps) za kufuatilia literacy & numeracy. | • Kuimarika kwa Stadi za msingi za KKK.<br><br>• Kuongezeka kwa mahusiano chanya kwa jamii.<br><br>• Uboreshaji wa mbinu za kufundishia kulingana na matokeo.<br><br>• Kuongezeka kwa mahudhurio na ushirikiano wa wanafunzi. |

| Na. | Mpango Mkakati | Mkakati Endelevu | Nyenzo | Matokeo |
|---|---|---|---|---|
| | | za KKK kwa ufanisi.<br>• Kuendeleza uwezo wa walimu na wasimamizi kutumia TEHAMA katika kupanga ufundishaji na kupima maendeleo ya watoto.<br>• Kuwezesha upatikanaji wa ripoti sahihi na haraka kwa Shule, Kata na Mikoa. | | |
| 6. | **Mazingira Wezeshi ya Ujifunzaji na Ustawi wa Mtoto** | • Kuweka miundombinu shuleni inayowezesha ujifunzaji na inayolinda usalama wa mtoto.<br>• Kutoa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa kuzingatia umri na mahitaji ya watoto.<br>• Kuhakikisha usafi, mwanga, mzunguko wa kutosha wa hewa pamoja na utoshelevu wa vifaa vya kuchezea na kujifunzia.<br>• Kutengeneza ratiba shuleni zinazochangia ustawi wa mtoto, ikiwemo mapumziko, michezo na mazungumzo ya kijamii. | • Madarasa yenye mwanga wa kutosha na hewa safi.<br>• Vyumba vya michezo na maeneo ya kujifunzia nje yenye usalama na muundo unaovutia.<br>• Mabango ya kielimu, ramani za rangi, picha zinazohamasisha maadili na chati za maendeleo ya watoto.<br>• Walimu wenye ujuzi wa malezi ya mtoto.<br>• Wazazi wanaoshiriki katika malezi, matukio ya kielimu na ushauri wa maendeleo ya mtoto. | • Kuongezeka kwa ustawi wa kisaikolojia na hisia za watoto.<br>• Uboreshaji wa matokeo ya kielimu.<br>• Kuongezeka kwa ushirikiano na mahusiano chanya. |

| Na. | Mpango Mkakati | Mkakati Endelevu | Nyenzo | Matokeo |
|---|---|---|---|---|
| | | • Kutoa msaada wa kihisia kwa watoto wanaopitia changamoto za kiBinafsi au familia.<br><br>• Kuanzisha programu za mshauri au waangalizi wa kijamii shuleni. | | |
| 7. | **Uongozi, Uratibu na Uendeshaji wa Utekelezaji** | • Kuhakiki kuwa viongozi wa shule na wasimamizi wa elimu wana uelewa wa kina wa Mkakati wa KKK.<br><br>• Kuendeleza uongozi unaohamasisha walimu na kuhimiza ubunifu katika ufundishaji.<br><br>• Kuhakikisha uongozi unashirikisha walimu, wazazi na jamii kufanya uamuzi wa maendeleo ya ujifunzaji.<br><br>• Kuanzisha na kuimarisha timu za uratibu shuleni (*School-Level Coordination Teams)*<br><br>• Kuweka ratiba za uratibu wa shughuli za ufundishaji, tathmini, mafunzo na mwendelezo wa ujifunzaji.<br><br>• Kutambua na kushughulikia changamoto za | • Miongozo ya kitaifa ya ufundishaji wa KKK.<br><br>• Mfumo wa miongozo ya uongozi wa kisayansi unaoshirikisha walimu, wasimamizi na jamii.<br><br>• Timu za usimamizi wa shule (school management teams).<br><br>• Timu za ufuatiliaji na tathmini za wilaya/mkoa.<br><br>• Ratiba za uratibu wa walimu, tathmini na mafunzo.<br><br>• Mfumo wa kuripoti maendeleo (*Reporting Templates*) kwa Shule, Kata, na Mkoa. | • Viongozi wa shule na wasimamizi wa elimu wanakuwa na uelewa thabiti wa malengo ya KKK na mikakati ya utekelezaji.<br><br>• Uongozi unakuwa shirikishi na unaohamasisha walimu, wazazi, na jamii kushiriki kikamilifu katika mpango wa KKK.<br><br>• Kuimarika kwa uwezo wa viongozi wa shule katika kusimamia, kuratibu na kufuatilia ufundishaji wa KKK.<br><br>• Viongozi wanatumia ushahidi na data kufanya maamuzi ya kitaaluma |

| Na. | Mpango Mkakati | Mkakati Endelevu | Nyenzo | Matokeo |
|---|---|---|---|---|
| | | utekelezaji kwa wakati unaofaa.<br><br>• Kujumuisha shughuli na mbinu za KKK katika miongozo na bajeti za shule na ngazi za kata/mkoa.<br><br>• Kuweka mifumo ya ufuatiliaji na tathmini endelevu ya utekelezaji wa KKK. | | yanayolenga kuboresha matokeo ya ujifunzaji. |

## MAREJELEO


African Union. (2016). Agenda 2063: The Africa we want. African Union Commission.

African Union. (2024). Continental education strategy for Africa (CESA) 2024–2034. African Union Commission.

Abdul Latif Jameel Poverty Action Lab. (2019). Teaching at the right level (TaRL): Evidence from randomized evaluations. J-PAL.

Chama Cha Mapinduzi. (2025). Ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) 2025–2030. Dodoma, Tanzania.

Food and Agriculture Organization of the United Nations. (2019). School food and nutrition framework. FAO.

Ha, T. T. T., Lien, V. T. T., & Hang, T. T. (2025). Early childhood education through a child-centered approach: Theoretical foundations and key issues. Macrolinguistics and Microlinguistics, 6(2), 74–84. https://doi.org/10.21744/mami.v6n2.40

Heckman, J. J. (2016). The economics of inequality: The value of early childhood education. American Educator, 35(1), 31–47.

National Examinations Council of Tanzania. (2021). Ripoti ya upimaji wa taifa wa Stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu kwa darasa la pili. NECTA.

National Examinations Council of Tanzania. (2022). Ripoti ya upimaji wa taifa wa Stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu kwa darasa la pili. NECTA.

National Examinations Council of Tanzania. (2023). Ripoti ya upimaji wa taifa wa Stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu kwa darasa la pili. NECTA.

UNESCO. (2021). Global education monitoring report: Early childhood care and education. UNESCO.

UNESCO Global Education Monitoring Report. (2020). Global education monitoring report 2020: Inclusion and education. UNESCO.

UNICEF. (2019). A world ready to learn: Prioritizing quality early childhood education. UNICEF.

United Nations. (2015). Transforming our world: The 2030 agenda for sustainable development. United Nations.

United Nations Development Group. (2017). UNDAF companion guidance: Theory of change. United Nations Development Group.

United Republic of Tanzania, Ministry of Education, Science and Technology. (2023). Education and training policy (2014, revised edition 2023). Government of Tanzania.

United Republic of Tanzania, Prime Minister's Office. (2021). National multisectoral early childhood development programme (NM-ECDP). Government of Tanzania.

United Republic of Tanzania, Tume ya Mipango. (2025). Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050. Ofisi ya Rais.

United Republic of Tanzania. (2025). Mpango wa maendeleo ya sekta ya elimu (ESDP) 2025/26–2029/30. Government of Tanzania.

World Bank. (2018). World development report 2018: Learning to realize education's promise. World Bank.

World Bank. (2020). Measuring learning poverty. World Bank.

World Bank. (2022). Ending learning poverty: What will it take? World Bank.

World Food Programme. (2024). Global school feeding report 2024/2025. WFP.

